# DHIMA YA TASWIRA KATIKA NYIMBO ZA MUZIKI WA KIZAZI KIPYA: MIFANO KUTOKA KWA NASIBU ABDUL NA MRISHO MPOTO

**SARAH MGALULA**

**SHAHADA YA UMAHIRI KATIKA FASIHI YA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA DODOMA**

**DISEMBA, 2020**

# DHIMA YA TASWIRA KATIKA NYIMBO ZA MUZIKI WA KIZAZI KIPYA: MIFANO KUTOKA KWA NASIBU ABDUL NA MRISHO MPOTO

NA

SARAH MGALULA

TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UMAHIRI KATIKA FASIHI YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA DODOMA

DESEMBA, 2020

## IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi, Sarah Mgalula, ninathibitisha kwamba tasinifu hii ni yangu asilia na kwamba, haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri au Shahada nyingine yoyote.

Saini 

Hairuhusiwi kuiga, kuchapisha, kutoa nakala, kutafsiri wala kusambaza sehemu yoyote ya tasinifu hii kwa namna yoyote ile bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

## ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasinifu hii inayoitwa '**Dhima ya Taswira katika Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya: Mifano kutoka kwa Nasibu Abdul na Mrisho Mpoto'**; na anapendekeza ikubaliwe kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

…………………………

Dkt. Zuhura A. Badru

(Msimamizi)

Tarehe 01/12/2020

## SHUKURANI

Kwa moyo wa dhati, ninamshukuru Mungu Muumba wa Mbingu na nchi kwa kunijaalia afya njema na kunipa uwezo wa kufanya utafiti, kuandika na kuikamilisha tasinifu hii.

Shukurani za kipekee ziende kwa msimamizi wangu, Dkt. Zuhura A. Badru, kwa kukubali kuwa msimamizi wangu. Yeye alikuwa mshauri, mwelekezaji na mwalimu aliyenikosoa na kunielekeza kwa busara na hekima kubwa kila ilipohitajika. Sina cha kumlipa lakini namuombea kwa Mwenyezi Mungu amzidishie moyo wa upendo na ampe nguvu zaidi ili aweze kuendelea kuwa hazina kubwa yenye kutegemewa kusudi wanufaike wengi wa enzi hizi na zijazo. Aidha, ninaushukuru uongozi mzima wa Chuo Kikuu cha Dodoma, hasa walimu waliopo katika Ndaki ya Insia na Sayansi za Jamii kwa kunifundisha, kunishauri mpaka kukamilika kwa tasinifuthii.

Shukurani za dhati ni kwa Mama yangu mpenzi, Bi. Mary David Mgalula, na dada yangu, Ruth. Asanteni sana kwa kunilea, kunisomesha, kunishauri na kuendelea kuwa rafiki wema na wa kweli katika maisha yangu. Nawapenda sana, mwenyezi Mungu aendelee kuwatunza na kuwabariki.

Shukurani maalum ni kwa mume wangu mpendwa, Bwa. Emmanuel Paschal, na watoto wangu wapenzi kwa kunitia moyo, kunivumilia na kunisaidia katika kipindi chote kigumu nilichokuwa nafanya utafiti mpaka kukamilisha tasinifu hii. Nawashukuru niliowataja kwa niaba ya wale ambao sikuwataja. Nyote nawaambieni asanteni sana.

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa watoto wangu wapendwa, Careen Emanuel, Colin Emanuel na Emanuela Emanuel, ili iwe kwao chachu ya kuthamini elimu na kujifunza kwa bidii.

## IKISIRI

Tasinifu hii ni matokeo ya utafiti uliochunguza Dhima ya Taswira katika Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya: Mifano kutoka kwa Nasibu Abdul (Diamond Platinum) na Mrisho Mpoto (Mjomba). Utafiti huu uliongozwa na malengo matatu mahsusi ambayo ni kubainisha taswira zinazojitokeza katika nyimbo za waimbaji teule, kujadili dhima ya taswira katika nyimbo za waimbaji teule na kutathmini athari za taswira katika nyimbo za waimbaji teule. Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni semiotiki kupitia misingi miwili kama ilivyofafanuliwa katika utafiti huu.

Utafiti ulifanyika uwandani na maktabani. Eneo la utafiti lilihusisha mkoa wa Dodoma na Dar es salaam. Data zilikusanywa kwa njia ya uchunguzi matini na usaili ambapo sampuli ilijumuisha vijana wenye umri kati ya miaka 17 hadi 35, madijei na wanafunzi wa shahada ya kwanza katika fasihi ya kiswahili. Aidha, matini zilizochunguzwa zilihusisha nyimbo za wasanii teule ambazo kwazo taswira zilibainishwa.

Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa, nyimbo za waimbaji teule zimesheheni matumizi ya taswira, hivyo, kuwezesha kubainishwa kwa taswira zilizojitokeza katika nyimbo teule. Miongoni mwa taswira zinazojitokeza ni pamoja na jongoo, ngongoti, roboti, chumvi, samaki, fisi, kibakuli cha vumba, ngalawa, mwiba, kuku, chui, roho, nzi, kuni, ugali, nyumba na vyumba. Aidha, dhima tulizozibaini ni pamoja na kukwepa udhibiti, kufikisha ujumbe, kuonesha ufundi wa msanii, kuvutia hadhira, kuburudisha hadhira, na kupamba kazi ya msanii. Pia, athari chanya za matumizi ya taswira ni kuibua hisia za hadhira, hukuza udadisi wa hadhira, kukua kwa kipera husika, hufanya maudhui yaeleweka kwa urahisi na kudumisha maadili ya jamii. Na athari hasi ni pamoja na kusababisha ugumu katika kupata undani wa maudhui yanayokusudiwa, kuchochea mmomonyoko wa maadili na pia kusababisha utata wa maana. Mchango mpya wa tasinifu hii ni kuonesha dhima ya matumizi ya taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya kama mbinu mojawapo ya utunzi wa kazi za kifasihi. Aidha, utafiti umependekeza tafiti nyingi zaidi ziendelee kufanyika katika eneo hili la taswira katika muziki wa kizazi kipya ili kuisheheneza zaidi fasihi simulizi ya Kiswahili.

**YALIYOMO**

IKIRARI NA HAKIMILIKI .................... i
ITHIBATI YA MSIMAMIZI .................... ii
SHUKURANI .................... iii
TABARUKU .................... iv
IKISIRI .................... v
YALIYOMO .................... vi
VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA .................... ix

**SURA YA KWANZA .................... 1**
**UTANGULIZI WA JUMLA .................... 1**
1.1 Utangulizi .................... 1
1.2 Ufafanuzi wa Dhana na Istilahi za Msingi .................... 1
1.2.1 Taswira .................... 1
1.1.2 Muziki wa Kizazi Kipya .................... 2
1.3 Historia na Chimbuko la Muziki wa Kizazi Kipya .................... 2
1.4 Usuli wa Tatizo la Utafiti .................... 2
1.5 Tamko la Tatizo la Utafiti .................... 4
1.6 Malengo ya Utafiti .................... 5
1.6.1 Lengo Kuu .................... 5
1.6.2 Malengo Mahususi .................... 5
1.7 Maswali ya Utafiti .................... 5
1.8 Manufaa tarajiwa ya Utafiti .................... 6
1.9 Mawanda ya Utafiti .................... 6

**SURA YA PILI .................... 7**
**MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA .................... 7**
2.1 Utangulizi .................... 7
2.2 Mapitio ya Maandiko .................... 7
2.2.1 Mapitio ya Maandiko Yanayohusu Taswira .................... 7
2.2.2 Mapitio ya Maandiko Yanayohusu Muziki wa Kizazi Kipya .................... 10
2.2.3 Mapengo ya Maarifa .................... 12
2.3 Kiunzi cha Nadharia iliyotumika .................... 12

2.4 Muhtasari wa Sura ya Pili ........ 15

**SURA YA TATU ........ 16**

**METHODOLOJIA YA UTAFITI ........ 16**

3.1 Utangulizi ........ 16

3.2 Usanifu wa Utafiti ........ 16

3.3 Eneo la Utafiti ........ 16

3.4 Walengwa wa Utafiti ........ 17

3.4.1 Wango la Utafiti ........ 17

3.4.2 Sampuli na Usampulishaji ........ 17

3.5 Mchakato wa Kukusanya Data ........ 19

3.5.1 Zana na Njia za Kukusanyia Data ........ 19

3.5.2 Vifaa vya Ukusanyaji na Kuhifadhia Data ........ 21

3.6 Mbinu za Uchambuzi na Uwasilishaji wa Data ........ 21

3.6.1 Mbinu ya Uchambuzi wa Data ........ 21

3.6.2 Uwasilishaji wa Data ........ 21

3.7 Itikeli za Utafiti ........ 21

3.8 Uhalali na Uthabiti wa Utafiti ........ 22

3.9 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake ........ 22

**SURA YA NNE ........ 24**

**UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI ........ 24**

4.1 Utangulizi ........ 24

4.1.1 Historia ya Wasanii na Muhtasari wa Nyimbo Teule ........ 24

4.1.2 Historia Fupi ya Mrisho Mpoto ........ 28

4.2 Taswira Zinazojitokeza katika Nyimbo za Waimbaji Teule ........ 31

4.2.1 Taswira Zinazojitokeza katika Nyimbo za Nasibu Abdul ........ 31

4.2.2 Taswira Zinazojitokeza katika nyimbo za Mrisho Mpoto ........ 37

4.3 Dhima ya Taswira katika Nyimbo za Waimbaji Teule ........ 45

4.3.1 Kukwepa Udhibiti ........ 45

4.3.2 Kufikisha Ujumbe ........ 47

4.3.3 Kuonesha Ufundi wa Msanii ........ 48

4.3.4 Kuvutia Hadhira ........ 49

4.3.5 Kuburudisha Hadhira ........ 49
4.3.6 Kupamba Kazi za Msanii ........ 50
4.4 Athari za Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Waimbaji Teule ........ 51
4.4.1 Athari Chanya za Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Waimbaji Teule ... 51
4.4.2 Athari Hasi za Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya ........ 54
4.5 Muhtasari wa Sura ya Nne ........ 57

**SURA YA TANO ........ 58**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 58**
5.1 Utangulizi ........ 58
5.2 Muhtasari waTasinifu ........ 58
5.3 Hitimisho ........ 58
5.4 Mapendekezo ........ 59
5.4.1 Mapendekezo kwa Wasanii wa Muziki wa Kizazi Kipya ........ 59
5.4.2 Mapendekezo kwa Jamii ........ 59
5.4.3 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo ........ 60
**MAREJELEO ........ 61**
**VIAMBATANISHO ........ 66**

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| A.K.A | Anajulikana Kama |
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili Zanzibar |
| Bi. | Bibi |
| Bwa. | Bwana |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Tasinifu hii imejikita katika kuchunguza Dhima ya Taswira katika Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya. Taswira katika kazi ya fasihi, hususani ushairi, ni kipengele muhimu sana. Mashairi ya muziki wa kizazi kipya, kama ilivyo kwa aina nyingine za mashairi, yanadhihirisha matumizi ya taswira zenye shabaha tofauti tofauti. Aidha, maana ya taswira hizo zimekuwa zikipokelewa kwa mitazamo tofauti na wasikilizaji wa muziki huo. Hivyo, lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza dhima ya taswira katika mashairi ya muziki wa kizazi kipya. Nyimbo zilizochunguzwa katika utafiti huu ni zile zilizoimbwa na msanii Nasibu Abdul (a.k.a Diamond Platnumz), kuanzia sasa Diamond Platnumz, na Mrisho Mpoto (a.k.a Mjomba), kuanzia sasa Mjomba. Sehemu hii ya utangulizi inahusika na ufafanuzi wa dhana, usuli wa tatizo la utafiti, tamako la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, manufaa ya utafiti na mawanda ya utafiti.

## 1.2 Ufafanuzi wa Dhana na Istilahi za Msingi

Tasinifu hii imetumia istilahi mbalimbali ambazo ni muhimu kufafanuliwa ili kurahisisha uelewekaji wake. Katika sehemu hii, istilahi muhimu ambazo zimetumika katika utafiti huu zinazojumuisha taswira na muziki wa kizazi kipya zimefafanuliwa.

### 1.2.1 Taswira

Taswira ni kipengele cha lugha ambacho huvuta hisia za msikilizaji au msomaji na kumuundia picha akilini mwake. Wamitila (2003) anasema kuwa, taswira ni picha zinazotokana na maelezo ya mwandishi ya moja kwa moja au ya picha ambazo zinatoa maelezo ya ziada. Anabainisha aina kuu mbili za taswira, ambazo ni: taswira ishara na taswira maelezo. Kwa jumla, dhana ya taswira hufuatana ama kuambatana na matumizi ya tamathali za semi kama vile sitiari na tashibiha. Hivyo, katika tasinifu hii, tunatumia istilahi taswira kumaanisha picha zinazotoa maelezo ya ziada katika kazi ya fasihi.

### 1.1.2 Muziki wa Kizazi Kipya

Muziki wa kizazi kipya ni istilahi inayotumiwa kurejelea muziki wa Bongo Fleva na Bongo Hip Hop ambayo humaanisha muziki unaopendwa na vijana wa sasa, yaani kizazi kipya nchini Tanzania na katika Ukanda wa Afrika Mashariki.

## 1.3 Historia na Chimbuko la Muziki wa Kizazi Kipya

Muziki wa kizazi kipya ulianza kuingia nchini Tanzania miaka ya 1980. Ulianzishwa na vijana ambao walitoka katika familia zenye uwezo. Vijana hao wengi wao walikuwa wakisoma nje ya nchi na wengine walikuwa na ndugu waliokuwa wakiishi huko nje ya nchi (Majembe, 1998; Remes, 1999 na Venance, 2017). Hii ina maana kuwa vijana hao walivutiwa na aina ya muziki waliokuwa wakiusikiliza huko nje au katika santuri walizoletewa na ndugu zao waliokuwa wakiishi huko na huo ndiyo ukawa mwanzo wa muziki huu kuingia nchini. Muziki huu ulikabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa jamii kwa sababu ya lugha iliyotumika, midundo, mavazi na uongeaji wa wasanii wake. Wasanii waliokuwa wakiimba muziki huo walionekana kuwa na uongeaji ambao hauendani na kaida na desturi za Kitanzania. Wasanii wanaotajwa kuwa waasisi wa muziki huu ni pamoja na Salehe Jabir, Mr 2 Proud (Sugu), Adili Kumbuka, Lady Jay Dee na Stara Thomas. Baadhi ya makundi yalianzishwa kama vile: *Kwanza Unity, Underground Souls, Deplowmatz, Hard Blasters Crew na Ugly Face.*

Kutokana na mabadiliko ya wakati na mahitaji ya kijamii, muziki huu kwa sasa umeshamiri na kuwa muziki pendwa nchini Tanzania. Mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, utandawazi, kuanzishwa kwa vyombo binafsi vya habari na kurekodia muziki, kukua kwa teknolojia ya kurekodia muziki na njia za usambazaji wa muziki yamesababisha kupendwa na kusambaa zaidi kwa aina hii ya muziki. Aidha, ubunifu wa baadhi ya wasanii na kuanza kuzungumzia matatizo ya jamii ndiyo chachu ya mafanikio ya muziki huu.

## 1.4 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Lugha ni kipengele muhimu sana katika kazi ya fasihi kwani ni nyenzo ambayo msanii huitumia kubeba maudhui na kuyawasilisha kwa hadhira yake. Kama ilivyo kwa kazi nyingine za ushairi, nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya nazo zimesheheni vipengele mbalimbali vya lugha. Baadhi ya vipengele vinavyotumika katika nyimbo

za muziki huu ni; taswira, lugha ya majigambo, lafudhi mbalimbali, misemo, tashtiti, tanakali sauti, misimu, sitiari, tashihisi na tashibiha (Omari, 2006; Jilala, 2010; na Venance, 2017).

Matumizi ya lugha katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya na kazi zingine za fasihi yameshughulikiwa na kutafitiwa na wataalamu mbalimbali na kwa namna tofauti. Kwa mfano, Majembe (1998) anaeleza kuwa nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya zimetawaliwa na uchanganyaji wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Anafafanua kuwa sababu kubwa inayowasukuma wasanii kuchanganya lugha ni kasumba waliyonayo wasanii katika kuiga Umarekani na kujidai kuwa wanajua Kiingereza na hata kuivutia hadhira ambayo wengi wao ni wazungumzaji wa lugha hiyo. Madai haya ya Majembe yanaungwa mkono na Fenn na Perullo (2000) ambao pia wanafafanua kuwa Muziki wa Kizazi Kipya umetawaliwa na uchanganyaji lugha katika nyimbo zake. Hata hivyo, tofauti na fikra za Majembe, wao wanaeleza kuwa uchanganyaji huo wa lugha unasababishwa na athari za kikoloni na mfumo wa elimu nchini Tanzania, ambao hutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Hili linatupa kubaini kuwa uteuzi wa lugha ya kutumia katika mashairi haufanywi tu kwa nasibu bali kuna sababu zinazoongoza mchakato huo.

Omari (2009) anasema kuwa miongoni mwa sababu za mashairi ya Muziki wa Kizazi Kipya (*Hip Hop*) kuwa fasihi pendwa ni matumizi ya lugha. Hii ina maana kuwa lugha inaweza kuijenga kazi ya fasihi ama kuibomoa/kuidhoofisha. Mathalani, Mzee (2011) anasema kuwa athari izipatazo jamii kutokana na matumizi ya lugha, zimechangia muziki wa taarab kupoteza asili yake na kuharibu maadili ya jamii. Hata muziki huu wa kizazi kipya huko nyuma ulikuwa ukipigwa vita kutokana na sababu mbalimbali (Mahenge, 2010 na Venance, 2017). Jamii iliuona muziki huu kuwa ni wa kihuni usiozingatia maadili ya Kitanzania na Kiafrika. Aidha, ulionekana kwamba unapotosha vijana na hata vijana waliokuwa wakiushabikia muziki huu walionekana kama watu waliokata tamaa ya maisha.

Kwa sasa muziki huu si tu kwamba unapendwa na vijana, bali pia ni muziki ambao umevuta hisia na kushabikiwa na watu wengi wa jinsi na rika mbalimbali, kutokana na kuenea na kukua kwa kasi ndani na nje ya mipaka ya Tanzania. Hali hii inatokana

na ukweli kwamba muziki huu umekuwa ukiburudisha, ukielimisha na ukielezea matatizo yanayoigusa jamii moja kwa moja.

Tafiti nyingi zilizofanyika kuhusu nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya zimechunguza masuala ya dhamira, matumizi ya lugha katika kuibua dhamira mbalimbali, muziki ulivyoingia na kupokelewa, ulivyoenea na mabadiliko uliyoyapitia. Hata hivyo, hakujawa na utafiti wa kina kuhusu dhima za taswira katika Muziki wa Kizazi Kipya na athari zake kwa jamii. Kwa mfano, Majembe (1998) alifanya utafiti kuhusu matumizi ya lugha katika muziki wa *Hip Hop* lakini kipengele cha taswira hakikushughulikiwa kwa kina. Aidha, Omari (2006) alichunguza mitindo na matumizi ya lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya Tanzania, ambapo kipengele cha taswira alikigusia kwa kifupi sana.

Tafiti nyingine ni kama, Samwel (2012) ambaye alifanya utafiti kuhusu mabadiliko katika majigambo alichunguza majigambo ya jadi na ya Bongo Fleva. Katika utafiti huu pia kipengele cha taswira kiligusiwa kwa ufupi sana. Vilevile, Selanda (2018) alifanya utafiti katika nyimbo za singeli na kuchunguza vionjo vya kisasa huku kipengele cha taswira kikiachwa. Naye, Venance (2017) alifanya utafiti kuhusu dhamira za kisiasa katika mashairi ya *Hip Hop* na jinsi zinavyoakisi jamii. Pamoja na ubora wa utafiti huu bado kipengele cha taswira hakikugusiwa kabisa kwani hakikuwa sehemu ya malengo ya utafiti tajwa. Kwa jumla, tafiti nyingi za awali hazikukizungumzia kwa kina kipengele cha taswira katika Muziki wa Kizazi Kipya pamoja na dhima zake, jambo ambalo limempa mtafiti mwanya wa kulishughulikia. Hivyo, utafiti uliozaa tasinifu hii umejikita katika kuchunguza dhima za taswira katika nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya, kwa kubainisha taswira zinazojitokeza katika nyimbo za wasanii teule na kuzitolea maana. Aidha, umefafanua dhima za matumizi ya taswira hizo na mwisho umeangazia athari za matumizi ya taswira katika Muziki wa Kizazi Kipya.

### 1.5 Tamko la Tatizo la Utafiti

Taswira ni kipengele chenye umuhimu sana katika kuipamba kazi ya kifasihi, hasa katika ushairi. Taswira hutumika kuzinasa hisia za hadhira kwani huwa na maneno yaliyopangwa kiufundi na yanayounda picha akilini mwa hadhira. Kama ilivyo kwa mashairi ya aina nyingine, nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya zimesheheni

matumizi ya taswira. Pamoja na umuhimu wa taswira, tunaona kuwa hakuna tafiti zilizojiegemeza kwa kina kutafiti suala la taswira katika Muziki wa Kizazi Kipya. Hali hii imsababisha kutokuwa na utoshelevu wa kimaarifa kuhusu matumizi ya taswira katika Muziki wa Kizazi Kipya. Aidha, hali hii huenda imesababisha pia kutoeleweka kwa ukamilifu kwa Muziki wa Kizazi Kipya.

Kutokana na hali hiyo, mtafiti alijiuliza maswali yafuatayo. Mosi, hivi taswira katika nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya zina maana gani? Pili, taswira katika nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya zina dhima yoyote faafu kama ilivyo katika mashairi ya aina nyingine? Mwisho, ni athari zipi zipatikanazo kutokana na matumizi ya taswira katika nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya? Maswali haya yalimpa msukumo mtafiti katika kuchunguza na kufafanua Dhima ya Taswira katika Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya, ili kuonyesha umuhimu wa matumizi ya taswira kama kipengele kimojawapo katika matumizi ya lugha. Mtafiti alimakinikia katika nyimbo za Nasibu Abdul na Mrisho Mpoto.

## 1.6 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu moja na malengo mahususi matatu: malengo haya ndiyo yamemwongoza mtafiti kufikia hitimisho la utafiti huu.

### 1.6.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhima ya taswira katika nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya.

### 1.6.2 Malengo Mahususi

Utafiti ulikusudia kutimiza malengo mahususi yafuatayo:

(i) Kubainisha taswira zinazojitokeza katika nyimbo za waimbaji teule;
(ii) Kujadili dhima ya taswira katika nyimbo za waimbaji teule, na;
(iii) Kueleza athari za taswira katika nyimbo za waimbaji teule.

## 1.7 Maswali ya Utafiti

Ili kukamilisha malengo mahususi yaliyoanishwa katika utafiti huu, mtafiti ameongozwa na maswali yafuatayo:

(i) Taswira zipi zinazojitokeza katika nyimbo za waimbaji teule?
(ii) Taswira zinazopatikana katika nyimbo za waimbaji teule zina dhima gani?
(iii)Taswira zinazopatikana katika nyimbo za waimbaji teule zina athari gani?

### 1.8 Manufaa tarajiwa ya Utafiti

Utafiti huu una faida zifuatazo: mosi, kuongeza maarifa kuhusu dhima ya taswira katika nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya. Pili, utafiti huu utasaidia kuonesha athari za taswira katika nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya kwa jamii. Tatu, utafiti huu utatumika kama marejeleo kwa tafiti zijazo. Nne, kufafanua dhima za taswira na kuonesha umuhimu wake katika usanaji wa nyimbo na fasihi kwa jumla.

### 1.9 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu ulihusu kuchunguza dhima ya taswira katika muziki wa kizazi kipya, kwa kujikita katika nyimbo za Daimond Platinumz na Mrisho Mpoto. Jumla ya nyimbo tano (5) kutoka kwa kila msanii zimetumika katika kukamilisha malengo ya utafiti huu. Hivyo kufanya jumla ya nyimbo kumi. Nyimbo nyingine za wasanii hawa na wasanii wengine zimegusiwa kwa jicho la jumla kwa lengo la kukazia maarifa. Nyimbo hizo zimechaguliwa kutokana na utumiaji mkubwa wa taswira katika kufikisha ujumbe kwa hadhira. Utafiti ulijikita katika kubainisha, kujadili na kueleza dhima za taswira katika nyimbo teule.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Utafiti uliozaa tasinifu hii ulihusu dhima za taswira katika muziki wa kizazi kipya. Utafiti wetu ulijikita katika kubainisha taswira zilizotumika katika nyimbo teule, dhima pamoja na athari za matumizi yake. Katika sura hii, tumefafanua mapitio ya maandiko na iunzi cha nadharia, masuala muhimu katika ufanyikaji wa utafiti. Vilevile, sura hii imebainisha mapengo ya maarifa yaliyobainika na kutoa maelezo ya jinsi mapengo hayo yalivyoshughulikiwa. Masuala hayo yanafafanuliwa katika kipengele 2.2 hadi 2.4 kama ifuatavyo:

## 2.2 Mapitio ya Maandiko

Sehemu hii inabainisha maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti. Katika sehemu hii, tumefafanua maandiko kuhusu dhana ya taswira na pia ni maandiko kuhusu Muziki wa Kizazi Kipya kama ifuatavyo:

### 2.2.1 Mapitio ya Maandiko Yanayohusu Taswira

Kuna tafiti na maandiko mbalimbali kuhusu taswira ambayo yamekwisha kuandikwa hadi sasa. Miongoni mwa hayo ni TUKI (2011) ambayo inaeleza kuwa taswira ni sawa na picha ya kitu iliyomo kichwani mwa mtu. Taswira hunasa hisia za wasomaji na wasikilizaji wa kazi ya fasihi kwa kuumba picha ya kitu akilini mwa mtu. Matumizi ya picha kwa asilimia kubwa huambatana na tamathali za usemi, ambazo ni vifananisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti zisizofanana. Andiko hili limetoa mwanga kwa mtafiti kuhusu dhana ya taswira. Maarifa haya yamesaidia kwa kiwango kikubwa katika ubainishaji wa taswira zinazojitokeza katika nyimbo za waimbaji teule na kuwezesha kufafanua dhima na athari za taswira.

Wamitila (2003) anafafanua kuwa taswira zimejengeka katika maumbo mbalimbali ambayo hutoa maana tofautitofauti kulingana na mwandishi anavyozichora ili kutoa maana iliyokusudiwa. Anazigawa taswira katika makundi mawili: taswira za kiishara na taswira za kimaelezo. Ijapokuwa Wamitila amejikita zaidi katika fasihi andishi lakini ufafanuzi wake umeonesha wazi kuwa, kazi za fasihi hutumia kwa kiasi kikubwa mbinu ya taswira ili kuvuta hisia za msomaji au msikilizaji. Hivyo, andiko

hili limeweza kumwongoza mtafiti katika kuzichambua taswira mbalimbali zinazojitokeza katika nyimbo teule na kufafanua dhima za taswira hizo.

Naye, Senkoro (1982) anafafanua kuwa taswira ni lugha inayochora picha ya vitu au mahali kwa kutumia ishara. Anafafanua zaidi kuwa matumizi ya taswira humsababishia msomaji au msikilizaji kuvutiwa na kazi husika kwani taswira ni kama pambo katika kazi za fasihi. Taswira ndizo zitoazo hisi mbalimbali za kunusa, kusikia, kuona, kuonja na kugusa. Hivyo, anazigawa taswira katika aina tatu ambazo ni; taswira zionekanazo, taswira za mawazo na taswira za hisi. Mawazo haya ya Senkoro yametoa msaada na kuutajirisha utafiti wetu, na hasa katika kubainisha taswira zinazojitokeza katika nyimbo teule na kuwezesha ufafanuzi wa dhima za taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya.

Masungwa (2012) alifanya utafiti kuhusu taswira na ishara katika ushairi wa Mathias Mnyampala na kubainisha aina mbalimbali za taswira na ishara zilizojitokeza katika ushairi wa Mnyampala. Aidha, mtafiti huyo anaeleza namna taswira na ishara hizo zinavyoibua maudhui katika kazi za Mnyampala. Pamoja na utafiti wa Masungwa kujikita katika fasihi andishi, lakini umetupatia maarifa ya kutosha ambayo yamesaidia sana katika katika utafiti huu kwani utafiti wake umetoa ufafanuzi kuhusu aina za taswira, umuhimu wa taswira na kuonesha namna ya kubainisha taswira na ishara katika ushairi. Mawazo haya yamekuwa ni mwongozo katika kubainisha taswira zinazojitokeza katika nyimbo teule na kisha kufafanua dhima na athari za matumizi ya taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya.

Tandiko (2015) alichunguza dhima ya taswira katika nahau za Kisambaa. Katika utafiti wake, aliweza kubainisha taswira mbalimbali zinazojitokeza katika nahau za Kisambaa na kufafanua athari na uhusiano uliopo baina ya taswira zilizomo kwenye nahau na maisha halisi ya jamii. Katika utafiti wake, hakujihusisha na dhima za taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya. Hata hivyo, utafiti wake unahusiana sana na utafiti huu na umetoa mwanga na mwelekeo kuhusu umuhimu wa taswira katika kazi za fasihi, hasa fasihi simulizi. Maarifa haya yametusaidia katika kufafanua dhima ya taswira kama zinavyojitokeza kwenye nyimbo za muziki wa kizazi kipya.

Badru (2011) alitafiti kuhusu dhima ya taswira na mabadiliko yake katika vitendawili vya Kiswahili. Katika utafiti wake alionesha namna taswira za vitendawili vya Kiswahili zinavyobadilika kutokana na mabadiliko yanayotokea katika jamii. Utafiti huu unahusiana sana na utafiti wetu na umetoa mwelekeo na maarifa zaidi kuhusu dhana ya taswira. Vilevile, umesaidia katika kubaini dhima za taswira na namna zinavyojitokeza katika kazi za fasihi, na hasa fasihi simulizi, suala ambalo tumelishughulikia katika utafiti huu. Mtaalamu huyu amejigeza zaidi katika suala la vitendawili na kutojishughulisha na dhima ya taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya kwa kuwa halikuwa tatizo lake la utafiti, hivyo kutoa mwanya ambao umezibwa na utafiti huu.

Aidha, Badru (2015) alitafiti kuhusu taswira na ubainishaji wa mabadiliko ya kiujumi katika vitendawili vya Kiswahili. Humo alibaini namna ambavyo taswira zinawezesha uwasilishaji wa amali za jamii kupitia vitendawili na kufafanua nafasi ya taswira katika kufanya maamuzi ya kiujumi kwenye vitendawili vya Kiswahili. Utafiti huu umekuwa chachu kubwa katika utafiti wetu kwa sababu umetoa maarifa ya kutosha kuhusu matumizi ya taswira na athari zake katika ufasiri na uelewekaji wa vitendawili kwa hadhira. Mwanazuoni huyu alishughulikia mabadiliko ya kiujumi katika vitendawili vya Kiswahili lakini hakujihusisha na dhima ya taswira katika muziki wa kizazi kipya. Hata hivyo, maarifa ya andiko lake yametusaidia sana katika kufafanua taswira zinazojitokeza katika nyimbo teule na athari zake.

Halikadhalika, Mwari (2016) alifanya uchambuzi kuhusu matumizi ya taswira za hali katika nyimbo za kizazi kipya na kufafanua maana mbalimbali zinazowasilishwa na taswira hizo. Katika uchambuzi wake huo, anaeleza kuwa wasanii wanazungumzia masuala ya ngono, ulawiti, ubakaji, ndoa, talaka na suala kuu la UKIMWI kupitia matumizi ya taswira mbalimbali katika utunzi wa nyimbo zao. Utafiti huu umesaidia kupata maarifa ya awali kuhusu matumizi ya taswira katika muziki wa kizazi kipya. Hata hivyo, utafiti huu haukushughulika na dhima ya taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya na hivyo kutoa mwanya ambao umezibwa katika utafiti huu.

Vilevile, Kasege (2013) alifanya utafiti kuchunguza namna matumizi ya lugha yanavyoibua dhamira za kisiasa katika diwani ya *Fungate ya Uhuru* (1998) na *Wasakatonge* (2003). Katika ufatiti wake huo, alishughulikia vipengele vya lugha

kama: taswira, sitiari, kejeli, chuku, tashihisi, takriri, nidaa, ishara, majigambo na misemo. Pamoja na kwamba utafiti huu haukujikita katika muziki wa kizazi kipya, lakini uchunguzi wake katika matumizi ya lugha umesaidia kumwongezea maarifa mtafiti kuhusu dhima ya taswira inavyosaida kuibua dhamira.

Simon (2014) alichunguza kuhusu ishara katika *Kaptula la Marx* na *Kijiba cha Moyo* kwa kugemea mtazamo wa kisimiotiki. Pamoja na mambo mengine, alibaini kuwa matumizi ya ishara hutatiza katika upatikanaji wa ujumbe na hivyo kuathiri maana inayowasilishwa. Japokuwa mtafiti huyu amejikita zaidi katika fasihi andishi na kuchunguza suala la ishara, bado andiko lake linahusiana sana na utafiti huu kwa sababu ishara zipatikanazo katika kazi ya fasihi husababisha msomaji au msikilizaji kupata au kujenga picha fulani akilini mwake (taswira). Utafiti huu umetupatia maarifa ya awali kuhusu athari za matumizi ya ishara ikiwa inashabihiana na lengo letu la tatu ambapo ni kueleza ni athari zipi zitokanazo na matumizi ya taswira katika nyimbo za kizazi kipya.

### 2.2.2 Mapitio ya Maandiko Yanayohusu Muziki wa Kizazi Kipya

Wataalamu wengi wametafiti na kuzungumzia kuhusu nyimbo za muziki wa kizazi kipya. Mathalani, Fenn na Perullo (2000) waliangalia uteuzi wa lugha katika muziki wa *Hip Hop* ya Tanzania na Malawi. Walibaini kuwa, kuna uchanganyaji wa lugha katika muziki huo. Katika *Hip Hop* ya Tanzania walionesha kuwa kuna matumizi makubwa ya uchanganyaji wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili na walifafanua kuwa uchanganyaji huu unasababishwa na athari za kikoloni na mfumo wa elimu nchini Tanzania. Mfumo huu unatumia lugha mbili, Kiswahili na Kiingereza, ambapo wasanii wengi wamepita katika mfumo huu na kuathiriwa. Pia, wanaeleza kuwa nyimbo zinazotumia lugha ya Kiingereza husheheni maudhui ya wasanii kujisifia wao wenyewe na marafiki zao. Wakati zile zinazotumia lugha ya Kiswahili hubeba maudhui yanayozungumzia masuala muhimu yanayogusa jamii. Utafiti huu wa Fenn na Perullo haukujikita katika dhima ya taswira, lakini umetoa maarifa ya jumla na kuonesha namna matumizi ya lugha yalivyo na umuhimu katika kuibua maudhui kwa jamii. Hivyo, kutokana na andiko hili tumepata maarifa kuwa dhima ya taswira, kama kipengele kimojawapo katika matumizi ya lugha, ni kubeba maudhui fulani yaihusuyo jamii.

Halikadhalika, Omari (2006) amefanya uchambuzi wa mitindo na matumizi ya lugha katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya. Pamoja na taswira, mitindo mingine ya lugha inayotumika katika muziki huu ni matumizi ya lafudhi, lugha ya majisifu, misimu, misemo na methali. Ingawa mtafiti huyu ameshughulikia muziki wa kizazi kipya lakini hakugusia kipengele cha taswira, hasa dhima na athari za matumizi ya taswira. Hivyo, kuacha mwanya ambao umezibwa na utafiti wetu. Hata hivyo, utafiti wake umetusaidia kupata maarifa ya awali kuhusiana na vipengele mbalimbali vya lugha vinavyotumika katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya. Katika vipengele hivyo vya lugha tumemakinikia kipengele cha taswira na kuchunguza dhima na athari za matumizi ya taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya.

Aidha, Omari (2009) alifanya utafiti akichunguza mambo yaliyochochea ushairi wa Hip Hop ya Kiswahili kuwa miongoni mwa fasihi pendwa. Katika utafiti huu amebaini kuwa kupendwa kwa muziki huu kunasababishwa na mitindo na matumizi ya lugha pamoja na vipengele vingine vya kifani na kimaudhui. Uchambuzi wa Omari umetoa hamasa kwa kuonyesha namna lugha inavyoweza kuvutia makini ya wasikilizaji wa muziki wa kizazi kipya. Taswira kama mojawapo ya mbinu katika usanaji wa kazi za fasihi husaidia kuvuta hisia za hadhira, kwani huifanya hadhira kujenga picha akilini mwake na kupata hisia mbalimbali kuhusu kazi hiyo ya kifasihi. Andiko hili lina umuhimu sana katika utafiti wetu kwani limetoa msaada katika kuchunguza athari za matumizi ya taswira kama kipengele kimojawapo cha lugha. Ingawa Omari alijikita zaidi katika kuchunguza vipengele vya lugha lakini hakuangazia dhima ya taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya. Hivyo, kutoa mwanya ambao umezibwa na utafiti wetu.

Pia, Jumbe (2015) alifanya utafiti kuhusu matumizi ya lugha katika muziki wa kizazi kipya kwa kujikita kwenye nyimbo za mapenzi. Utafiti huu ulilenga kubainisha lugha inayotumika katika kusawiri vionjo vya mapenzi pamoja na athari ambazo hadhira hupata. Utafiti huu umebaini kuwa, lugha inayotumiwa katika muziki wa kizazi kipya huteuliwa kutokana na sababu mbalimbali miongoni mwa sababu hizo ni: soko la muziki, mapenzi ya wasanii wenyewe katika tungo za mapenzi na kuonesha hisia kwa wapenzi wao. Utafiti wa Jumbe umetajirisha utafiti wetu kwa namna mbalimbali. Kwanza, umetupa maarifa kuhusiana na historia hususani chimbuko la muziki wa kizazi kipya, lakini pia, umetupa maarifa kuhusu matumizi

ya lugha, taswira ikiwa kama kipengele kimojawapo. Mtaalamu huyu aliangazia matumizi ya lugha katika nyimbo za mapenzi lakini hakuangazia kuhusu dhima ya taswira katika nyimbo hizo. Hivyo, utafiti wetu umeziba mwanya huo.

Naye, Venance (2017) alifanya utafiti kuhusu dhamira za kisiasa katika mashairi ya Muziki wa Kizazi Kipya hususani Bongo Hip Hop na jinsi zinavyoakisi jamii. Pamoja na kwamba katika utafiti wake ameangalia dhamira, lakini pia ameangalia na mitindo ya lugha inavyosaidia kuibua dhamira hizo. Mitindo ya lugha aliyoishughulikia ni kama vile: tashibiha, sitiari, kejeli, tashihisi, msemo, misimu, takriri, ishara na mgotanisho. Mtafiti huyu ameshughulikia muziki wa kizazi kipya pasipokugusia kipengele cha taswira, hivyo, kutoa mwanya kwa utafiti wetu.

### 2.2.3 Mapengo ya Maarifa

Baada ya kupitia baadhi ya maandiko tumebaini kuwa tafiti nyingi zilizofanyika kuhusiana na muziki wa kizazi kipya zimejikita kwenye vipengele vingine vya lugha na kipengele cha taswira kutomakinikiwa. Aidha, tafiti mbalimbali zilizogusa dhana ya taswira zilijikita zaidi katika fasihi andishi, huku fasihi simulizi ikichunguzwa kwa uchache. Hivyo, ili kuziba pengo lililojitokeza, utafiti huu umechunguza Dhima ya Taswira katika Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya.

## 2.3 Kiunzi cha Nadharia iliyotumika

Wafula na Njogu (2007) wanafafanua nadharia kuwa ni maelezo ya jambo kufungamana na vigezo vilivyowekwa au vinavyozalika kutokana na majaribio ya jambo hilo. Kutokana na ufafanuzi huo, tunatambua kwamba ni lazima kuwepo kwa vigezo maalumu katika kusoma au kusikiliza kazi za kifasihi. Vigezo hivyo humwezesha msomaji au msikilizaji kuielewa kazi husika. Hivyo, nadharia ya semiotiki imetumika katika tasinifu hii kuchunguza dhima ya taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya.

Semiotiki ni nadharia ya kihakiki ambayo inajishughulisha na uchunguzi wa ishara na alama kwa kuangalia uhusiano wake na kitu husika. Wamitila (2002) anaeleza kuwa neno semiotiki asili yake ni neno la Kigiriki ‘semeion’ lenye maana ya ishara. Wanaendelea kufafanua kuwa neno hili lenye maana ya ishara hutumiwa kuelezea mielekeo au mitazamo ya makundi fulani ya kihakiki. Kwa msingi huu,

wanasemiotiki huangalia ishara kwa kuhusianisha uhusiano wake na kitu husika katika kazi za fasihi.

Suala la ishara na uashiriaji kama mtindo wa kuhakiki kazi za kifasihi unaoshughulikia matumizi ya ishara limeanza kuwa muhimu kama nadharia ya uhakiki wa kifasihi mnamo karne ya 20 hususani miaka ya 1970. Kipindi ambacho kulikuwa na vuguvugu kubwa la kuasi na kuachana na nadharia ya umuundo ambayo ilikuwa imetawala uhakiki wa kifasihi katika miaka ya 1960. Mwanaisimu wa ki-Swizi Ferdinand de Saussure na mwanafalsafa wa kipragmatiki wa Marekani Charles Sanders Peirce ni miongoni mwa wanaotajwa kuwa ni waasisi wa nadharia hii, wakati Roman Jacobson, Voloshnov, Bakhtin, Derrida, Umberto Eco, Greimas, Todorov, Kristeva na Roland Barthes ni wataalamu waliokuja kuipa mashiko ama kuisukuma nadharia hii ya semiotiki ambayo wataalamu wengine huiita semiolojia (Hawkes,1977; Selden, 1985 na Wamitila, 2002).

Wataalamu mbalimbali wa isimu na fasihi wameeleza kuhusu maana ya semiotiki. Mathalani, Wamitila, (2003) akitoa ufafanuzi wa kifasihi kuhusu nadharia hii, anasema semiotiki ni aina ya nadharia ya kimuundo inayojishughulisha na ishara na maana za ishara hizo katika kazi za kifasihi. Anaendelea kusema kuwa, nadharia hii kimsingi huangazia uashiriaji na jinsi kazi za kifasihi zinavyowasiliana na wasomaji. Ni nadharia ambayo huchunguza sababu zinazofanya kazi za kifasihi ziwe na maana zilizo nazo kwa wasomaji wa kazi hizo. Hivyo, ni lazima ziwepo sababu za msomaji ama msikilizaji wa kazi za kifasihi kupata maana kutokana na matumizi ya ishara ama taswira katika kazi husika kwa kurejelea na mazingira halisi iliyomo hadhira husika.

Aidha, Masamba (2004) akitoa ufafanuzi wa kiisimu anafafanua kuwa semitotiki ni taaluma ya kisayansi inayojishughulisha na uchunguzi na uchanganuzi wa mifumo ya ishara mbalimbali ikiwa inazingatia zaidi uhusiano baina ya kiwakilishi na kiwakilishwa. Kutokana na ufafanuzi wa Massamba, tumebaini kuwa maana ya kitu inapatikana kwa kuangalia uhusiano uliopo baina ya kitaja (kiwakilishi) na kitajwa (kinachowakilishwa).

Vilevile, Wafula na Njogu (2007) wanaona semiotiki ni taaluma ya mipangilio ya ishara inayomwezesha binadamu kuona vitu au hali kama ishara zenye maana. Wataalamu hawa huona kuwa nadharia ya semiotiki huangazia masuala ya ishara, matumizi ya ishara na matumizi ya lugha kwa jumla katika kazi za kifasihi.

Kimsingi, nadharia hii hushughulikia neno kama kiwakilishi cha kile kinachotajwa. Hii inamaanisha kuwa, maana ya kitu au jambo inaweza kupatikana kupitia taswira zitokanazo na ishara. Hivyo, nadharia hii ya semiotiki ni nadharia ya uhakiki wa fasihi inayojishughulisha na uchungunzi wa ishara au alama kwa kuangalia uhusiano wake na wa kitu au jambo husika.

Chandler (2005) anafafanua kuwa, katika kufasiri ishara au kupata maana ya ishara, lazima mambo matatu yafanyike. Mosi, ishara na dhana ihusishwe na uelewaji wa mtu kuhusu ishara fulani. Pili, dhana na kitajwa ihusishwe na tajriba aliyonayo mtu kuhusu ishara. Mwisho, ishara na kitajwa vihusishwe  na kanuni na utamaduni wa jamii husika. Mawazo haya ya Chandler ni muhimu kwa tasinifu hii kwa kuwa yatatusaidia kupata maana ya taswira zilizomo katika kazi za wasanii teule kwa kuzingatia mambo hayo matatu.

Barthes (1968) anaitaja misimbo mitano ya uelewaji kwenye uhakiki wa ishara katika kazi za kifasihi ambayo hutumika kama mihimili mikuu katika nadharia ya semiotiki. Misimbo hiyo ni mosi, msimbo wa matukio. Pili, msimbo wa kiheminiki huu ni msimbo unaohusishwa na taharuki na usimulizi. Pia, huitwa msimbo wa kusimulia ambao huweza kufumbwa kwenye jina la kazi ya fasihi. Tatu, msimbo wa ki-seme, huu ni msimbo ambao unaohusisha elementi nasibishi za kisemantiki ambazo hutuonyesha picha ya mhusika fulani wa kifasihi. Nne, msimbo wa kiishara, huu ni msimbo unaohusishwa na namna wasomaji wanavyotambua na kufafanua maana za ishara katika kazi za kifasihi. Mwisho ni msimbo wa kiurejelezi, huu ni msimbo unaoundwa au kuhusishwa na viashirii vya kiutamaduni ambavyo vinarejelewa katika kazi za kifasihi. Aidha, msimbo huu huhusisha matumizi ya vitu fulani ambavyo vinaeleweka na wasomaji/wasikilizaji wa kazi za fasihi na hivyo kuipa kazi fulani nguzo ya kiutamaduni.

Ingawa nguzo zote katika nadharia hii ni za muhimu, lakini utafiti huu umetumia msimbo au nguzo mbili tu ambazo ni msimbo wa kiishara na msimbo wa kiurejelezi katika kuchanganua Dhima za Taswira katika Nyimbo za Wasanii Teule wa Muziki wa Kizazi Kipya. Misimbo hii miwili ilichaguliwa kwa sababu inashabihiana na mada ya utafiti. Aidha, inahusisha namna wasomaji/wasikilizaji wanavyotambua na kufafanua maana za ishara katika kazi za kifasihi. Misimbo hii imetuongoza katika tasinifu hii na imesaidia katika kujibu maswali ya utafiti na kisha kutimiza malengo bainifu ya tasinifu hii. Kupitia nadharia hii, tumegundua kuwapo kwa matumizi makubwa ya taswira ambazo zimeweza kuchanganuliwa. Taswira zilizomo katika nyimbo teule zimechunguzwa na kubainisha maana, dhima na athari zake katika muziki wa kizazi kipya.

## 2.4 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura hii imepitia tafiti na machapisho mbalimbali na nadharia iliyotumika katika utafiti huu. Mapitio yaliyopitiwa ni yale yanayohusu taswira na muziki wa kizazi kipya. Tafiti na machapisho hayo ndiyo yameibua mwanya kwa utafiti huu na kumhamasisha mtafiti kuchunguza Dhima ya Taswira katika Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya. Sura inayofuata inahusu methodolojia ya utafiti iliyotumika katika utafiti huu.

# SURA YA TATU

# METHODOLOJIA YA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Utafiti wetu ulihusu Dhima za Zaswira katika Muziki wa Kizazi Kipya, ambapo zinaanza kubainishwa taswira zilizojitokeza katika nyimbo teule; zinaelezwa dhima na matumizi yake, na; kufafanuliwa athari za taswira katika nyimbo teule. Sura hii ya tatu, inawasilisha ufanyikaji wa utafiti, yaani mbinu mbalimbali za utafiti, ukusanyaji na uchambuzi wa data na masuala mengine husianifu. Hivyo, katika sura hii tumefafanua vipengele kama vile: usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanya data, mbinu za uchambuzi wa data na uhalali na kuaminika kwa mbinu za utafiti. Vipengele hivyo vinafafanuliwa katika 3.2 hadi 3.8 kama ifuatavyo.

## 3.2 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mpango wa kazi wa jumla wa namna ya kufanya utafiti (Kothari, 2004). Ili kukidhi malengo ya tasinifu hii, mtafiti amekusanya data uwandani na maktabani. Maktabani data zilikusanywa na kuchanganuliwa kwa kutumia mbinu ya uchunguzi matini. Matini ambazo zilichanganuliwa maktabani zilijumuisha matini za sauti (nyimbo teule za wasanii teule) na matini mbalimbali za kimaandishi kuhusiana na mada ya utafiti huu. Data za uwandani zilikusanywa kwa njia ya usaili kwa watafitiwa mbalimbali. Watafitiwa hao ni: Wataalamu wa fasihi, Madijei (wapigaji wa muziki wa kizazi) na wasikilizaji wa nyimbo za wasanii teule. Data katika utafiti huu zimechambuliwa na kuchanguliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo yaani mkabala usio wa kiidadi**.** Mkabala usio wa kiidadi ni njia ya kuchambua data katika muundo wa maelezo pasipo kufuata taratibu za kitakwimu (Kothari, 2004). Hivyo, matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kwa njia ya maelezo.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika katika mkoa wa Dodoma na Dar es Salaam. Mkoa wa Dodoma ulichaguliwa kwa sababu kuna maktaba kubwa iliyomsaidia mtafiti kupata maandiko mbalimbali yaliyowezesha kupata data za tasinifu hii. Aidha, utafiti katika mkoa wa Dar es Salaam ulifanyika katika wilaya ya Kinondoni na Ubungo. Wilaya hizi zilichachaguliwa kwa sababu ndiko wanakoishi wasanii teule na kilipo Chuo

Kikuu cha Dar es Salaam ambacho kina maktaba kubwa na makavazi ambayo yametusaidia katika mapitio ya maandiko. Aidha, mikoa hii ina vijana wengi ambao ni wasikilizaji na mashabiki wa nyimbo za muziki wa kizazi kipya ambao pia walisaidia upatikanaji wa data za tasinifu hii.

## 3.4 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu wamegawanywa katika wango tafitiwa na sampuli ya watafitiwa.

### 3.4.1 Wango la Utafiti

Wango ni kundi la watu, matukio na vitu ambako sampuli ya utafiti huteuliwa (Kothari, 2004). Data ya tasinifu hii zilipatikana kutoka katika makundi yafuatayo:

a. Nyimbo mbalimbali za wasanii Nasibu Abdul na Mrisho Mpoto. Nyimbo hizi zimetumika katika kubainisha taswira, kutathimini na kufafanua dhima na athari za taswira katika muziki wa kizazi kipya.
b. Wanafunzi wa mwaka wa pili wa shahada ya kwanza katika fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma.
c. Wasikilizaji mbalimbali wa nyimbo za muziki wa kizazi kipya
d. *Madijei* ambao ni wapigaji wa muziki wa kizazi kipya.

### 3.4.2 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ni sehemu ya wango ambayo imeteuliwa ili itumike katika kusaka majibu ya tatizo. Usampulishaji ni kitendo cha kuteua sehemu ndogo ya wango ili itumiwe na mtafiti katika kuchunguza na kupata majibu ya tatizo lake la utafiti (Ponera, 2019). Tasinifu hii imetumia usampulishaji wa aina mbili, ambao ni usampulishaji nasibu na ule usio wa kinasibu (lengwa)

#### 3.4.2.1 Usampulishaji Nasibu

Humaanisha mchakato wa kuteua sampuli ambao unatoa fursa sawa ya kutafitiwa kwa kila kitafitiwa kilichomo kwenye wango la utafiti (Ponera, 2019). Kwa jumla, usampulishaji nasibu hufanyika kwa kutumia mbinu kadha wa kadha, kama vile; kubahatisha, kupangilia au kutabakisha. Katika tasinifu hii, usampulishaji nasibu ulitumika katika kuteua nyimbo kumi na tano (15) kutoka kwa kila mwimbaji lengwa ili kuzisikiliza. Jedwali lifautalo linaonesha nyimbo hizo:

**Jedwali Na. 1.1: Nyimbo za Waimbaji Teule Zilizosikilizwa Kupata Sampuli Lengwa:**

| | JINA LA MSANII | |
|---|---|---|
| **Na.** | **Diamond Platnumz** | **Mrisho Mpoto** |
| 1 | Nimwambie (2010) | Nikipata nauli (2010) |
| 2 | Ntampata Wapi (2011) | Gongo la Mboto (2014) |
| 3 | Ntarejea( 2012) | Samahani Wanangu (2014) |
| 4 | Kesho (2013) | Waite (2015) |
| 5 | Kizaizai (2013) | Njoo uichukue (2015) |
| 6 | Nataka Kuolewa (2013) | Deni la hisani (2015) |
| 7 | Nimoende Nani (2013) | Chocheeni kuni (2015) |
| 8 | Nasema nawe (2015) | Adela (2015) |
| 9 | Ukimuona (2015) | Asanteni kwa kuja (2015) |
| 10 | Salome (2017)) | Uhuru wangu (2015) |
| 11 | Sikomi (2018) | Sizonje (2016) |
| 12 | Iyena (2018)) | Kitendawili (2017) |
| 13 | Kanyaga (2019) | Nimwage radhi (2018) |
| 14 | Baba lao (2020) | Nenda salama Ruge (2019) |
| 15 | Jeje (2020) | Kwaheri Corona (2020) |
| **JUMLA** | **15** | **15** |

Baada ya kuzisikiliza nyimbo husika usampulishaji lengwa ulitumika ili kupata nyimbo tano (5) kwa kila mwimbaji. Lengo kuu la kuteua nyimbo hizo ilikuwa ni kukidhi malengo husika ya tasinifu hii na hivyo haikutakiwa kuchunguza na kuchambua nyimbo zote 30.

#### 3.4.2.2 Usampulishaji Lengwa

Usampulishaji huu huwa hautoi nafasi au fursa sawa ya kutafitiwa kwa sababu mtafiti humakinikia kundi fulani la vitu au watu ambao ana uhakika kuwa atapata taarifa zinazoakisi malengo ya utafiti. Japokuwa wapo waimbaji wengi wa Muziki wa Kizazi Kipya, mtafiti aliamua kuwatumia wasanii wawili tu wa kiume: Diamond Platnumz na Mrisho Mpoto. Sababu kubwa ya mtafiti kuwateua waimbaji hawa, ilikuwa umashuhuri wao, nyimbo zao kusheheni taswira zilizoweza kukidhi matakwa

ya tasinifu hii, pamoja na uwakilishi wa uimbaji tofauti, ambapo Nasibu Abdul yeye anaimba huku Mrisho Mpoto akighani kwa sehemu kubwa.

Nyimbo tano (5) kwa kila msanii ziliteuliwa kupata sampuli lengwa. Kwa upande wa Diamond Platnumz nyimbo hizo ni: Nasema Nawe (2015); Salome (2017); Iyena (2018); Sikomi (2018); na Kanyaga (2019). Nyimbo za Mrisho Mpoto ni: Njoo Uichukue (2015); Chocheeni Kuni (2015); Waite (2015); Sizonje (2015) na Kitendawili (2017). Nyimbo hizi ziliteuliwa kutokana na utafiti wa awali kuonesha kuwa zina data zinazohusiana na utafiti huu na hivyo kutoa taarifa madhubuti.

Aidha, vijana ishirini na mbili (22), wa kike kumi na moja (11) na wa kiume kumi na moja (11), wenye umri kati ya miaka kumi na saba mpaka thelathini na tano (17 - 35) kutoka katika mkoa wa Dodoma na Dar es Salaam, ambao ni wasikilizaji wa muziki wa kizazi kipya waliteuliwa. Lengo likiwa ni kupata maoni yao juu ya matumizi ya taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya. *Madijei* watano (5) kwa sababu ndio wapigaji wakuu wa nyimbo za muziki wa kizazi kipya katika walipendekeza maeneo mbalimbali. Vilevile, wanafunzi kumi (10) wa mwaka wa pili wa shahada ya kwanza katika fasihi ya Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Wanafunzi hao walichaguliwa kutokana na ubobevu wao katika fasihi ya Kiswahili. Hivyo, walitoa mchango na mawazo ya kutosha kuhusu dhima ya taswira na athari za taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya.

Kwa jumla, walengwa wa utafiti wametusaidia kwa kiasi kikubwa katika kubainisha taswira zinazojitokeza katika nyimbo teule, kisha kufafanua dhima na athari za matumizi ya taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya.

### 3.5 Mchakato wa Kukusanya Data

Sehemu hii inafafanua njia na zana zilizotumika kwenye ukusanyaji na uwasilishaji wa data.

#### 3.5.1 Zana na Njia za Kukusanyia Data

Katika tasinifu hii, mtafiti amekusanya data za aina mbili: data za msingi na data fuatizi. Data za msingi zilikusanywa kutoka nyimbo za Nasibu Abdul na Mrisho Mpoto ambazo zilipatikana kwa kusikiliza nyimbo za waimbaji teule. Pia, data kutoka katika vyanzo kama majarida, vitabu na makala mbalimbali nazo zilitumika

katika kufanikisha upatikanaji wa taarifa zilizohitajika. Njia hii imemsaidia mtafiti kubainina kufahamu kwa urahisi taswira zinazojitokeza katika nyimbo teule. Data fuatizi ni data ambazo mtafiti alikusanya kutoka kwa wanafunzi, *Madijei* na Wasikilizaji wa muziki wa kizazi kipya. Data hizi zilichanganuliwa na kushadidia data za msingi. Mbinu zifuatazo zilitumika katika ukusanyaji wa data:

#### 3.5.1.1 Usaili

Usaili ni njia ya kukusanya data kwa kuhusisha mazungumzo baina ya mtafiti na mtafitiwa kuhusu jambo ambalo mtafiti anakusudia kulipata (Kombo na Tromp, 2006). Kwa ujumla, njia hii huhusisha mazungumzo baina ya mtafiti na mtafitiwa katika kutafuta majibu ya malengo yake maalumu. Usaili unaweza kufanyika kwa namna mbili kuu: usaili wa moja kwa moja au usaili wa kidigitali (matumizi ya simu). Kupitia mbinu hii, mtafiti aliweza kubaini taswira zinazojitokeza katika nyimbo teule, athari za matumizi ya taswira na dhima ya taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya. Njia hii imechaguliwa na imetumika kwa sababu inampa mtafitiwa uhuru wa kutoa majibu na ilimwezesha mtafiti kupata data alizozihitaji. Katika njia hii, mtafiti aliweza kuuliza maswali ya nyongeza na kutoa ufafanuzi wa maswali hayo pale ilipohitajika. Njia ya usaili ilitumika kukusanya data za wanafunzi wa mwaka wa pili wa shahada ya kwanza katika fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma, *madijei* na wasikilizaji wa nyimbo teule waliochaguliwa. Kwa kutumia stadi nzuri za mawasiliano, hasa katika kuzungumza na kusikiliza, mtafiti aliweza kupata taarifa alizozihitaji.

#### 3.5.1.2 Uchunguzi Matini

McKee (2001:140) anasema, “Textual analysis is a methodology in a way of gathering and analyzing information in academic research” yaani “Uchunguzi matini ni njia mojawapo inayotumiwa na watafiti katika kukusanya na kuchanganua taarifa za utafiti wa kitaaluma” (tafsiri yetu). Ukusanyaji na uchanganuzi wa data hizo huweza kuwa katika maandishi au sauti. Lengo kuu la uchunguzi matini ni kubaini maudhui ya ujumbe uliomo katika matini husika. Katika tasinifu hii, uchunguzi matini ulifanyika katika matini sauti ambapo nyimbo teule za waimbaji Nasibu Abdul (Diamond Platinum) na Mrisho Mpoto zilizohifadhiwa katika sidii, kompyuta na maktaba za kidijiti hasa *youtube* zilisikilizwa na kuchunguzwa ili kuweza kubaini taswira zinazojitokeza katika nyimbo hizo. Aidha, dhima na athari za matumizi ya

taswira katika nyimbo husika ziliangaziwa. Mbinu hii ilitumika na hivyo kumsaidia mtafiti kupata data kwasi na za kina.

### 3.5.2 Vifaa vya Ukusanyaji na Kuhifadhia Data

Vifaa vilivyotumika kukusanyia na kuhifadhia data ni pamoja na sidii zilizohifadhiwa nyimbo za wasanii teule, kompyuta ambayo ilitumika kusikilizia nyimbo za wasanii teule na kuzinukuu pamoja na kupakua nyimbo za waimbaji teule na matini mbalimbali yaliyohifadhiwa mtandaoni. Kompyuta pia ilitumika kuhifadhi, kuchambua data na kuandikia taarifa ya utafiti. Shajara na kalamu vilitumiwa kunukuu nyimbo za waimbaji na taswira zinazojitokeza katika nyimbo zao kwa ajili ya uchambuzi. Aidha, kamera ya mnato na simu ya mkononi vilitumika. Vifaa hivi vilichaguliwa kwa kuzingatia aina ya watoa taarifa pamoja na mahitaji ya utafiti.

## 3.6 Mbinu za Uchambuzi na Uwasilishaji wa Data

Sehemu hii inahusu mbinu za uchanganuzi na uchambuzi wa data na uwasilishaji wake.

### 3.6.1 Mbinu ya Uchambuzi wa Data

Kothari (2004) anasema kuwa uchambuzi wa data ni mchakato wa kushughulikia data zilizopatikana kutokana na mchakato wa ukusanyaji ili ziweze kuleta matokeo yaliyokusudiwa. Uchambuzi wa data za tasinifu hii ulitumia mkabala wa kitaamuli. Mkabala kitaamuli ni mkabala ambao hutumika katika tafiti zisizohusisha tarakimu wakati wa ukusanyaji wa data (Ponera, 2019). Hivyo data za tasinifu hii zilihifadhiwa katika njia ya maelezo, kisha kuzifafanua kulingana na maelezo ya msingi yaliyotolewa na watafitiwa. Data zilizochambuliwa ni zile ambazo zinazoendana na malengo yaa utafiti husika.

### 3.6.2 Uwasilishaji wa Data

Kwa kuwa utafiti huu ni wa kitaamuli, uwasilishaji wa data umefanyika kimaelezo ambapo data zilizochanganuliwa zimewasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuzitolea ufafanuzi kama inavyodhihirika katika sura ya nne.

## 3.7 Itikeli za Utafiti

Utafiti wowote ule kuanzia hatua ya ukusanyaji, uchambuzi hadi uwasilishaji wa data huhitaji kuzingatiwa kwa misingi ya maadili ya utafiti. Utafiti huu umezingatia

suala la itikeli za utafiti kwa kuzingatia yafuatayo; kabla ya utafiti, mtafiti aliomba ridhaa ya Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya kukusanya data. Wakati wa utafiti, mtafiti alizingatia uaminifu katika kukusanya data kwa usahihi. Aidha, mtafiti alizingatia ukweli na usahihi katika uchambuzi wa data ili kuepuka udanganyifu katika matokeo ya utafiti huu.

### 3.8 Uhalali na Uthabiti wa Utafiti

Kwa mujibu wa Maxwell (1996) na Dey (2005) wanaeleza kuwa uhalali wa matokeo katika mkabala wa kitaamuli huhusisha hali ya kuaminika kwa maelezo, hitimisho, ufafanuzi, ufasili na aina yoyote ya maelezo yaliyotolewa. Ili utafiti uwe halali ni lazima uwe na uwezo kupima jambo linalotakiwa kwa uhakika na uwazi zaidi. Uthabiti wa utafiti ni ile hali ya utafiti kufanikisha kuleta matokeo yanayoendana, ikiwa utafiti huo utafanyika wakati mwingine, mahali pengine au hata kufanywa na mtu mwingine kwa mada ile ile. Hivyo, ili kupata uhalali na uthabiti wa utafiti huu, mtafiti ametumia mbinu tofauti tofauti katika kunukuu na kufanya uchanganuzi wa data katika ufikiaji wa matokeo sahihi ya utafiti. Mbinu hizo ni pamoja na: mtafiti kutumia njia mbili katika ukusanyaji wa data (usaili na uchunguzi matini). Vilevile, Lugha bainifu na rahisi ilitumika katika ukusanyaji wa data na utafiti ulifanyika bila upendeleo wa hali yoyote. Data zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Uchanganuzi wa data ulizingatia misingi na maelekezo ya nadharia ya semiotiki.

### 3.9 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake

Kukamilika kwa tasinifu hii, kumeambatana na changamoto mbalimbali ambazo mtafiti alikabiliana nazo. Changamoto kubwa ambayo imemwathiri mtafiti ni mlipuko wa Ugonjwa wa Virusi vya Korona 20019 kuanzia mwezi Machi hadi Julai. Changamoto kubwa iliyosababishwa na mlipuko huo ni ugumu wa kukutana na watafitiwa kwa wakati uliopangwa kwa kuzingatia masharti ya serikali. Mtafiti alitatua changamoto hii kwa kufanya usaili na baadhi ya watafitiwa kwa njia ya simu (usaili usio wa kuonana). Njia hii ilimsaidia mtafiti kukusanya data alizozihitaji kwa wakati unaofaa. Pili, utayari wa watafitiwa kuzungumzia mada ya utafiti ulikuwa katika kiwango duni sana. Baadhi ya watafitiwa, hasa wasikilizaji na wapigaji wa muziki hawakuwa tayari kuhojiwa na mtafiti moja kwa moja. Mtafiti alitatua changamoto hii kwa kuwaeleza faida ya utafiti huu na kuwahakikishia kuwa

matakwa ya watafitiwa katika kuwasilisha matokeo yangezingatiwa. Baada ya kupata uelewa watoa taarifa walikubali kufanyiwaa usaili.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Utafiti wetu ulihusu dhima za taswira katika muziki wa kizazi kipya mifano ikidondolewa kutoka kwa Nasibu Abdul na Mrisho Mpoto. Mtafiti alikusudia kubainisha taswira zilizotumika katika nyimbo teule, kueleza dhima za matumizi ya taswira hizo na athari zake katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia usaili na uchambuzi matini. Uchambuzi wa data ulizingatia nadharia ya semiotiki na data zilichambuliwa kwa kuzingatia mkabala wa kitaamuli. Katika sura hii tumewasilisha mjadala wa matokeo ya utafiti. Hivyo, sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza inatoa historia za wasanii na muhtasari wa nyimbo teule; sehemu ya pili imeonesha namna taswira zinavyojitokeza katika nyimbo teule; sehemu ya tatu inachambua dhima ya taswira katika nyimbo teule, na; sehemu ya nne inaeleza athari za taswira katika nyimbo teule.

### 4.1.1 Historia ya Wasanii na Muhtasari wa Nyimbo Teule

Kabla ya kuanza kufafanua taswira zilizobainika katika nyimbo teule, ni vema tukaanza kwa kutoa maelezo mafupi kuwahusu wasanii na nyimbo teule. Historia hii inaanza kwa kutolewa maelezo kumhusu msanii Nasibu Abdul na kufuatiwa na maelezo kumhusu Mrisho Mpoto kama inavyobainika katika kipengele 4.1.1.1 na 4.1.1.2.

#### 4.1.1.1 Historia Fupi ya Nasibu Abdul

Nasibu Abdul Juma alizaliwa tarehe 02/10/1989, katika hospitali ya Amana Dar es Salaam. Baba yake mzazi anaitwa Abdul Juma na mama yake anaitwa Bi. Sandra Kassim. Asili ya Nasibu Abdul (Diamond Platinumz) ni huko Kigoma japo amekulia Tandale katika jiji la Dar es Salaam ambako alikuwa akiishi na bibi yake mzaa mama, dada yake aitwaye Esma na mama yake mzazi. Mwaka 1995 alianza elimu yake ya chekechea katika shule ya Chakula Bora iliyopo Tandale, Uzuri hadi mwaka 1996. Alijiunga na shule ya msingi Tandale Magharibi iliyopo jijini Dar es Salaam na kuhitimu mwaka 2002. Katika mwaka 2003 alijiunga na shule ya sekondari na kuhitimu kidato cha nne mwaka 2006.

Kipaji cha Nasibu Abdul (Diamond Platinum) kilianza kujitokeza tangu mwaka 2000 akiwa darasa la tano, ambapo alikuwa akikariri nyimbo za wasanii mbalimbali wakongwe na kuziimba katika matamasha mbalimbali. Mnamo mwaka 2007, alijikita rasmi katika muziki wa kizazi kipya na kuanza kutunga nyimbo, ambapo mwaka 2009 alikutana na ndugu Msafiri Peter maarufu kama Papaa Misifa ambaye alijitolea kumsaidia kimuziki na kumwezesha kurekodi wimbo wake wa kwanza uliokuwa ukiitwa Nenda Kamwambie. Wimbo huu ulimpatia Diamond umaarufu na kuweza kubadilisha maisha yake. Mwaka 2010, alifanikiwa kuachia album yake ya kwanza iliyokuwa na nyimbo kumi. Hapo ndio umaarufu wa Diamond ukaongezeka na kusababisha ajulikane ndani na nje ya nchi ya Tanzania. Mpaka sasa, Diamond amefanikiwa kushinda tuzo mbalimbali kama vile: Tanzania Music Awards (2010 na 2013) na kuwa mwanamuziki bora wa kiume wa Bongo Fleva na msanii bora wa kiume wa wanamuziki wote Tanzania. Tuzo nyingine alizoshiriki ni BET Awards, MTV Europe na Channel O Awards. Msanii huyu ametoa mchango mkubwa sana katika muziki wa kizazi kipya na kuikuza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Tanzania.

#### 4.1.1.2 Muhtasari wa Nyimbo za Nasibu Abdul (Diamond Platinum

Kwa ujumla, nyimbo za Diamond Platinum zimesheheni kwa kiasi kikubwa masuala ya mapenzi na ndoa, akizungumza zaidi juu ya sifa za mwanamke bora anavyopaswa kuwa katika ndoa au mahusiano ya mapenzi. Haya yanadhihirika katika nyimbo teule ambazo ni “Iyena,” “Salome” na “Nasema nawe.” Aidha, amezungumzia suala la usaliti na ubinafsi katika wimbo wa “Sikomi” na “Kanyaga.” Katika kufikisha ujumbe kwa jamii, mwimbaji ametumia taswira mbalimbali ili kuvutia na kuipamba kazi yake. Katika sehemu hii tunawasilisha ufafanuzi wa nyimbo teule ili kurahisisha usomaji wa tasinifu hii.

##### 4.1.1.2.1 Iyena (ft.[1] Raymond Shaban Mwakyusa (Rayvanny)

Ni wimbo ulioimbwa na Nasibu Abdul mwaka 2018, akimshirikisha msanii mwenzake Rayvanny ambao wote wanatoka kwenye lebo ya WCB (*Wasafi Classic Baby*). Wimbo una jumla ya beti tano pamoja na kiitikio, na umefuata kanuni na sheria za mashairi ya kisasa ambayo hayazingatii kanuni za urari wa vina na mizani.

[1] Ft ni kifupisho cha Featuring, ikiwa na maana kuwa amemshirikisha msanii mwingine anayetajwa mbele ya kifupisho hicho.

Ubeti wa kwanza una mishororo 13, ubeti wa pili mishororo 14, ubeti wa tatu mishororo 5, ubeti wa nne mishororo 25 na ubeti wa tano una jumla ya mishororo 28. Wimbo huu umetumia taswira nyingi lakini maudhui yake kwa jumla yanahusiana na umuhimu wa kuoa au kuolewa. Kupitia wimbo huu, Diamond anajaribu kuwaasa wasiokuwa na ndoa kuachana na kasumba hiyo kwani ndani ya ndoa kuna raha. Aidha, anasisitiza suala la usafi wa mwanamke ndani ya nyumba. Kijumla, wimbo huu unatoa funzo kubwa kwa jamii yetu hasa wanandoa na wale wanaojiandaa kuingia katika ndoa.

#### 4.1.1.2.2 Salome (ft. Rayvanny)

Wimbo huu uliimbwa na Nasibu Abdul mwaka 2017 akishirikiana na msanii mwenzake Rayvanny ambao wako chini ya lebo ya WCB (*Wasafi Classic Baby*). Wimbo huu una jumla ya beti tano pamoja na kiitikio kimoja ambacho kimejitokeza. Wimbo huu mwanzo uliimbwa na msanii wa kike Saida Karoli hivyo kwa maelewano maalumu, Diamond aliurudia kwa kubadili beti za wimbo huo. Wimbo huu umejaa taswira nyingi kuanzia ubeti wa kwanza mpaka ubeti wa tano, kutokana na matumizi makubwa ya taswira wimbo huu umeivutia jamii kwa kiasi kikubwa, hivyo kuwa wimbo unaopendwa na kujulikana zaidi na watu rika zote katika jamii hasa ya Watanzania. Maudhui ya wimbo huu ni mapenzi baina ya mwanamke na mwanaume. Wimbo unasifia uzuri wa kufanya mapenzi mkiwa kwenye upendo wa dhati baina yenu, msanii anasisitiza watu wawe na mapenzi ya kweli na siyo ya kusalitiana.

#### 4.1.1.2.3 Sikomi

Wimbo huu uliimbwa na Nasibu Abdul mwaka 2018 ambaye ni msanii wa lebo ya WCB (Wasafi Classic Baby). Wimbo huu ameuimba peke yake pasipo kumshirikisha msanii yeyote. Wimbo huu aliutoa baada ya kuachana na mzazi mwenzie Zarinah Hassan (*Zari the boss lady*). Katika wimbo huu kuna jumla ya beti mbili ambazo zinafuatwa na kiitikio kila ukimalizika ubeti mmoja. Ubeti wa kwanza una jumla ya mishororo 21 ukifuatwa na kiitikio kisha kufuatwa na ubeti wa pili ambao una jumla ya mishororo 27. Katika wimbo huu mwimbaji amezungumzia maisha yake halisi hasa katika suala la mahusiano aliyowahi kuyapitia, katika wimbo huu amewataja baadhi ya wanawake aliowahi kuwa nao kwenye mahusiano. Maudhui ya wimbo huu ni ya mapenzi na usaliti. Anazungumzia namna ambavyo amekuwa akitendwa na

wapenzi wake aliowaamini na kuwapa kila kitu lakini bado walimsaliti na kumwacha. Maumivu mengi ameyapitia kutokana na kutendwa vibaya jambo ambalo linamsononesha. Yapo matumizi mengi ya taswira katika wimbo huu ambayo yanapatikana kwenye beti zote mbili.

#### 4.1.1.2.4 Kanyaga

Wimbo huu uliimbwa na msanii Nasibu Abdul mwaka 2019 anayetoka kwenye lebo ya WCB (*Wasafi Classic Baby*), katika wimbo huu hakushirikiana na msanii yeyote. Wimbo huu una jumla ya beti tisa, ambapo ubeti wa kwanza na wa pili zina mishororo 4 kwa kila mmoja, ubeti wa tatu na nne zina mishororo 5 kwa kila mmoja japo zimetenganishwa na kiitikio. Ubeti wa tano na sita zina mishororo minne minne kisha zimefuatwa na kiitikio. Ubeti wa saba na nane pia zina mishororo minne minne wakati ubeti wa tisa una mishororo mitano. Wimbo huu una taswira nyingi zilizotumika katika kufikisha ujumbe aliokuwa ameukusudia msanii kwa hadhira yake. Maudhui ya wimbo huu ni kuwasema wachonganishi, wambeya, vizabizabina na watu wengine waliozoea kuzungumza mambo yasiyowahusu. Pia unazungumzia watu ambao wamezoea kupata vitu pasipo kuvifanyia kazi, kwa namna hiyo tabia kama hizo zinapaswa kupingwa ndani ya jamii. Wimbo huu umeakisi maisha halisi katika jamii zetu tunazoishi, hivyo kwa ubunifu mkubwa na matumizi mazuri ya taswira katika kuisana kazi yake, mwimbaji amefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kuikemea jamii.

#### 4.1.1.2.5 Nasema Nawe

Huu ni miongoni mwa nyimbo alizoimba Msanii Nasibu Abdul mwaka 2015. Msanii huyu ambaye anatoka katika kundi linalomilikiwa na lebo ya WCB (*Wasafi Classic Baby*) lenye makao yake Dar es Saalam nchini Tanzania. Ameuimba wimbo huu akishirikiana na Khadija Kopa ambaye ni mwimbaji maarufu wa nyimbo za taarabu. Wimbo huu una jumla ya beti tatu ambazo zinatengwa na kiitikio kila unapokamilika ubeti mmoja. Ameanza kwa kiitikio kisha ukafuata ubeti kwa kwanza wenye mishororo 12 ambao umefuatwa na kiitikio. Ubeti wa pili una jumla ya mishororo 7 kisha kufuatwa na kiitikio. Ubeti wa tatu una jumla ya mishororo 6 ambayo imefuatwa na kiitikio. Maudhui ya wimbo huu yamejikita kwa wanawake ambao ni waongo na wambea, wanawake wa mazingira ya Uswahilini ambao kusutwa ni sehemu ya maisha yao. Wimbo unawaelekeza kuachana na uchonganishi kwani

hauna faida, hasara ambazo hutokana na umbeya ndani ya jamii ni nyingi kuliko faida.

### 4.1.2 Historia Fupi ya Mrisho Mpoto

Mrisho Mpoto alizaliwa tarehe 27/10/1978, huko Songea. Ni mtoto wa thelathini na sita kuzaliwa katika uzao wa baba yake Mzee Mpoto. Alipata elimu na kufanikiwa kuhitimu elimu yake ya msingi. Baada ya kuhitimu darasa la saba alianza kujishughulisha na ubebaji wa mizigo huko Iringa. Kwa kutumia elimu aliyoipata, alianza kusoma vitabu vya hadithi na kuwahadithia watu ambao walikuwa wakimlipa pesa. Hivyo, kumfanya Mrisho ajiongezee kipato chake cha siku. Katika shughuli zake alifanikiwa kupata pesa kwa ajili ya nauli na kuamua kwenda Dar es Salaam ambapo alijikita katika sanaa, hasa ya uimbaji wa mashairi.

Mrisho Mpoto amefanikiwa kuimba na kurekodi nyimbo mbalimbali. Kuna nyimbo alizoziimba peke yake, na zingine amewashirikisha wasanii wenzie kama vile: Banana Zoro, Harmonize, Diamond na wengineo. Nyimbo iliyomtambulisha na kumpa umaarufu kwa kasi ni ‘Nikipata Nauli’ ambayo ilivuta makini ya wasikilizaji ndani na nje ya nchi.

Kwa ujumla, amefanikiwa kupata tuzo mbalimbali katika muziki na mpaka sasa anamiliki kundi lake la muziki liitwalo Mpoto Theatre. Upekee wa mwimbaji huyu unajidhihirisha kwenye utunzi na uimbaji wa nyimbo zake kwani zimesheheni lugha ya taswira.

#### 4.1.2.1 Muhtasari wa Nyimbo za Mrisho Mpoto

Nyimbo za mwimbaji huyu zimejikita zaidi katika masuala ya siasa huku zikisheheni matumizi makubwa ya taswira. Matumizi hayo ya taswira yamemwezesha mwimbaji kufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa bila pingamizi kutoka katika mkono wa dola (serikali). Aidha, nyimbo zake humfikirisha msikilizaji na kwa namna anavyozisana nyimbo zake zinakuwa za kipekee na huweza kuvuta kwa urahisi makini za wasikilizaji.

##### 4.1.2.1.1 Waite

Wimbo huu umetungwa na kuimbwa na msanii Mrisho Mpoto mwaka 2015 ambaye anatoka katika lebo ya Mpoto Theatre Gallery. Wimbo huu una jumla ya beti mbili

na kiitikio. Msanii anaanza kwa kiitikio kisha unafuata ubeti wa kwanza wenye michororo 19 ambayo imezingatia utunzi wa mashairi ya kisasa yasiyofuata urari wa vina na mizani kisha kufuatwa na kiitikio. Ubeti wa pili unaundwa na mishororo 40 kisha unafuatwa na kiitikio ambacho kinatamatisha wimbo. Maudhui ya wimbo huu ni ujenzi wa jamii mpya, ambapo anapingana na uongozi mbovu uliojaa rushwa. Katika wimbo huu, Mpoto anamwambia kiongozi mwenye mamlaka kuwachunguza watendaji ndani ya serikali kisha wenye hatia wawajibike kwa kujihusisha na ulaji wa rushwa. Anasisitiza kuwa, asilimia kubwa ya viongozi wa umma wamejaa rushwa, hivyo kuwa chanzo cha kuchelewa kwa maendeleo ya Taifa. Wimbo huu umejaa matumizi mengi ya taswira katika uwasilishaji wa ujumbe aliokusudia mtunzi.

#### 4.1.2.1.2 Chocheeni Kuni

Huu ni wimbo wa msanii Mrisho Mpoto aliouimba mwaka 2014 akishirikiana na msanii mwenzake Ditto. Maudhui ya wimbo huu ni muendelezo wa mashairi yake yenye utata ambao ni utunzi wa hali ya juu katika kufumba maneno dhidi ya siasa ya Tanzania. Ujumbe wa wimbo huu ni kuhusu ujenzi wa jamii mpya, ambapo anauambia uongozi ulioko madarakani kuendeleza utendaji mbovu. Kuendelea kuwadanganya wananchi kwa mambo mbalimbali yasiyo ya kweli, ipo siku hawatakubaliana na uongo huo jambo litakaloleta matatizo ndani ya Taifa. Wimbo una jumla ya mashairi mawili na kiitikio ambacho kimeimbwa na Ditto. Ubeti wa kwanza una jumla ya mishororo 21 na ubeti wa pili una jumla ya mishororo 27. Mashairi ya wimbo huu yamezingatia sheria na kanuni za kisasa ambayo hayazingatii urari wa vina na mizani.

#### 4.1.2.1.3 Njoo Uichukue

Ni miongoni mwa nyimbo za Mrisho Mpoto kutoka lebo ya Mpoto Theatre Gallery ambao aliuimba mwaka 2015 akimshirikisha msanii mwingine ajulikanaye kwa jina la Felly Kano. Wimbo huu umejaa matumizi ya taswira nyingi, katika kufikisha ujumbe wake kwa jamii aliyokusudia. Kanuni na sheria alizozingatia katika utungaji wa beti za mashairi ya wimbo huu ni zile za kisasa ambazo hazizingatii kuwapo kwa urari wa vina na mizani. Maudhui ya wimbo huu ni ya siasa za Taifa letu, ambapo anasisitiza kuwa mafanikio mazuri kwa viongozi wa nchi ni kuachana na mambo ya ovyo ambayo hayana tija kwa wananchi. Anasisitiza viongozi kuepukana na rushwa

na badala yake watende yaliyo mema na yenye msingi kwa ustawi wa Taifa. Wimbo una jumla ya beti mbili zilizoimbwa na Mrisho Mpoto na kiitikio kilichoimbwa na Felly Kano. Ubeti wa kwanza una jumla ya mishororo 17 ilihali ubeti wa pili una jumla ya mishororo 19.

#### 4.1.2.1.4 Kitendawili

Wimbo huu uliimbwa na msanii Mrisho Mpoto kutoka kwenye lebo ya Mpoto Theatre Gallery mwaka 2017 akimshirikisha msanii wa muziki wa kizazi kipya Kassim Mganga. Wimbo una mashairi yanayozingatia kanuni za kimapinduzi yaani usasa yasiyofuata kanuni za urari wa vina na mizani. Maudhui ya wimbo huu ni ya kisiasa ambapo anawaonya wanasiasa kuachana na tabia zao mbovu, wanasiasa wamejaa uongo mwingi hasa wakati wa kampeni lakini wanapokwenda bungeni hujisahaulisha na kufanya mambo ambayo hawajatumwa na wananchi. Wanasiasa wanachangia kutokea kwa maafa wakati wa kampeni ambapo hupandikiza chuki dhidi ya wenzao, baadhi ya mashabiki wao hufikia hata kufa au kupata ulemavu kwa ajili ya kuwapambania lakini mwisho wa yote wanasiasa huwasahau. Wimbo una jumla ya beti tatu zilizoimbwa na Mrisho Mpoto na kiitikio ambacho kimeimbwa na Kassim Mganga kwa sehemu kubwa na sehemu ndogo Mrisho Mpoto. Ubeti wa kwanza una jumla ya mishororo 12, ubeti wa pili una mishororo 18 wakati ubeti wa tatu una mishororo 8.

#### 4.1.2.1.5 Sizonje

Mrisho Mpoto ni miongoni mwa watunzi bora na wenye weledi wa hali ya juu katika utunzi wa mashairi yanayotumia taswira ili kufikisha ujumbe aliokusudia ndani ya jamii. Wimbo wa Kitendawili aliuimba mwaka 2018. Kama ilivyo kawaida kwa maudhui ya nyimbo zake nyingi, Mpoto huwa ameegemea sana kwenye suala la siasa akilenga ujenzi wa jamii mpya. Katika wimbo huu anajaribu kuzungumza na viongozi wa juu katika Taifa, kufanya kazi kwa weledi akiwasisitiza kuwatumikia raia wao huku wakijitahidi kuhifadhi siri za ndani. Siyo vyema kila jambo linalofanyika ndani ya serikali ambalo halipaswi kufika kwa raia likawafikia; viongozi wanapaswa wawe na vifua vya kutunza siri. Pia katika wimbo huu, amewashauri waandishi wa habari kuwa makini na taarifa wanazozitoa kwani zingine zinapotosha jambo ambalo siyo zuri kwa ustawi wa Taifa. Wimbo huu una jumla ya beti mbili pamoja na kiitikio ambavyo vyote ameimba Mrisho Mpoto. Ubeti

wa kwanza una jumla ya mishororo 27 wakati ubeti wa pili una jumla ya mishororo 24. Wimbo wote umezingatia sheria na kanuni za utunzi wa mashairi ya kisasa ambayo hayazingatii kanuni na sheria za urari wa vina na mizani.

### 4.2 Taswira Zinazojitokeza katika Nyimbo za Waimbaji Teule

Katika sehemu hii tutawasilisha mjadala na matokeo ya utafiti kwa kujikita katika lengo la kwanza la tasinifu hii. Sehemu hii imegawanyika katika vipengele viwili: Kwanza, tumebainisha taswira zinazojitokeza katika nyimbo za Nasibu Abdul. Pili, Tutabainisha taswira zinazojitokeza katika nyimbo za Mrisho Mpoto.

#### 4.2.1 Taswira Zinazojitokeza katika Nyimbo za Nasibu Abdul

Katika utafiti huu imebainika kwamba nyimbo teule za Nasibu Abdul zina matumizi makubwa ya taswira. Miongoni mwa taswira zilizobainika ni pamoja na jongoo, ngongoti, roboti, chumvi, samaki, fisi, kibakuli cha vumba na ninga. Katika sehemu hii, tumezifafanua taswira hizo kama ifuatavyo:

##### 4.2.1.1 Jongoo

Jongoo ni mdudu ambaye anapatikana kwa kiasi kikubwa katika mazingira yetu ya kila siku. Kwa kawaida, huwa ni mweusi au wa kikahawia mwenye miguu mingi sana (TUKI, 2013). Sifa mojawapo ya mdudu huyu ni namna anavyojilinda anapokutana na adui. Jongoo hutumiwa kwenye kazi za fasihi kuashiria vitu mbalimbali kwa kuhusianisha na mazingira halisi. Wimbo wa "Salome" umetumia taswira ya jongoo katika beti zake kama inavyobainika katika ubeti ufuatao:

(1)

Mimi suruali yanidondoka,
Tukimbizane nini Salome wangu?
Iyo michezo ya jogoo,
Mbona watizama chini Salome wangu,
Ukimuona jongoo,
Inamana kidogo, shika magoti.

Muktadha wa wimbo umetumia taswira ya jongoo kufananisha na sehemu ya siri ya uzazi ya mwanamume. Mahusiano baina ya wahusika wawili (wa kike na kiume) yanatuongoza katika kupata taswira hiyo. Tabia na mwonekano wa sehemu ya uzazi ya mwanamume imelinganishwa na tabia ya jongoo. Matumizi ya taswira hii

yanaambatana na msemo wa Kiswahili ambao unasema ‘Jongoo hapandi mtungi.’ Msemo huu unaashiria namna ambavyo uume hausimami (jongoo); yaani hawezi kufanya mapenzi na mwanamke (mtungi). Kutokana na maelezo haya, namna msanii anavyomtumia jongoo katika wimbo wake, tunashawishika kuamini kuwa hii ni taswira yenye maana ya sehemu za siri za mwanamume.

#### 4.2.1.2 Ngongoti

Ngongoti ni mtu anayejivalisha miti mirefu miguuni na kuonekana na kimo kirefu sana kwa madhumuni ya kuvutia katika ngoma, kama vile: sindimba au michezo mingine (BAKIZA, 2010). Katika lugha ya Kiswahili, neno ngongoti hutumiwa kuonesha sifa apewazo mtu mrefu. Upande wa fasihi ya Kiswahili, ngongoti humaanisha sifa ya urefu uliopitiliza kwa binadamu. Msanii Diamond ametumia neno ngongoti kama taswira kwenye wimbo wa “Salome.” Tuangalie mfano wa taswira hiyo katika mistari ya ubeti huu:

(2)

> Inamana kidogo, shika magoti,
> Mimi nimesimama kama ngongoti,
> Mtoto jojo, siyo roboti.

Neno ngongoti limetumika kama taswira kuashiria kitu ambacho ni kirefu na kimesimama vizuri. Msanii anamwambia mpenzi wake aache aibu, ashike magoti maana yeye amesimama kama ngongoti. Taswira hii ni mwendelezo wa taswira ya jongoo. Tabia ya jongoo kulala na kuamka imeashiria tabia ya umbile la sehemu ya uzazi ya mwanamume. Taswira ya ngongoti imetumika kuonesha utofauti na nyongeza katika taswira ya jongoo. Taswira hii imetumika kuonesha namna ambavyo jongoo amesimama imara (sio fupi, bali ndefu). Ujumbe tunaoupata hapa unaendana na dhamira ya wimbo husika ambao unahusika zaidi na suala la ngono baina ya wahusika wawili. Hivyo, ngongoti imetumika kuonesha sehemu ya uzazi ya mwanamume ambayo imesimama imara ikitofautisha na jongoo wa kawaida.

#### 4.2.1.3 Roboti

Roboti ni kitu kinachotengenezwa kwa umbile la binadamu na kufanya matendo fulani mithili ya binadamu ambacho huendeshwa kwa mitambo au kwa programu maalumu za kompyuta (BAKIZA, 2010). Roboti hufanya mambo yote kwa matakwa

ya anayeiongoza na hazina sifa ambazo binadamu wa kawaida wanakuwa nazo. Sifa mojawapo ni kunyumbulika. Binadamu ana uwezo wa kunyumbua viungo vingi vya mwili wake, lakini roboti hazina uwezo wa kunyumbulika ama kujikunjakunja. Taswira hii imetumika katika wimbo wa “Salome” katika mistari ifuatayo:

(3)

Mimi nimesimama kama ngongoti,
Mtoto jojo, siyo roboti,
Chumbani bingilibingili sambasoti.

Neno roboti katika muktadha wa wimbo huu limetumika kuashiria kitu kisichokuwa na uwezo wa kunyumbulika na kuchezesha viungo vyake. Msanii anamsifia Salome kwa jinsi anavyonyumbulika katika mchakato wa kupeana mapenzi. Taswira hii ya roboti katika wimbo wa ‘Salome’ imetumika kumaanisha hali ya mwanamke kutoweza kunyumbulika katika mchakato wa kupeana raha (ngono). Kama tunavyoweza kuona katika mistari hii, msanii anaposema 'mtoto jojo, siyo roboti' ni lugha ya taswira ambayo anamsifia mchumba wake (mtoto) kuwa ni laini na ana uwezo wa kunyumbulika katika mitindo mbalimbali wakati wa kufanya mapenzi.

#### 4.2.1.4 Taswira ya Chumvi

Chumvi ni madini meupe ambayo hutiwa katika chakula wakati au baada ya kupika ili kuongeza ladha au utamu (TUKI, 2013). Chumvi hupewa thamani ndogo katika maisha yetu ya kila siku, ila thamani yake huwa ni kubwa sana inapokosekana. Neno hili huweza kutumiwa kuashiria maana mbalimbali (kama vile: kuongeza maneno ya ziada) katika mazungumzo ya kawaida na kwenye kazi za fasihi. Wasanii wengi hutumia neno hili kama taswira ya yale wanayomaanisha. Msanii Diamond pia ametumia neno hili kama taswira katika wimbo wa “Iyena:”

Asante mama ulinifunza nkajua,
Baba kasema kuomba mwiko,
Raha ya chumvi kununua,
Tena si kwa nazi,
Si hirizi za waganga,
Kwa baraka za baba na mama.

Jamii nyingi huzoea kuomba chumvi, hasa wakati wa mapishi. Mtunzi ametumia muktadha huu uliozoeleka kufikisha ujumbe wake kwa hadhira katika namna ambayo imejengwa kitaswira zaidi. Mazoea ya kuomba chumvi kila mara wakati wa

kupika hakumfanyi mwombaji kuwa huru kuitumia chumvi hiyo. Anaweza kupewa kidogo isitoshe kwa upishi au pia akapewa chumvi iliyoharibika ikaharibu ladha ya chakula chote. Hivyo, kuwa na chumvi humfanya mpishi awe huru juu ya utumizi wa chumvi hiyo.

Chumvi inapata maana yake kulingana na muktadha wa wimbo husika. Wimbo huu unahusu siku ya harusi, ambapo kijana anapata mke wa kuanza naye maisha. Anakumbuka maneno 'raha ya chumvi kununua,' maneno ambayo aliambiwa na baba yake. Chumvi katika muktadha wa wimbo huu imetumika kama 'mke,' yaani mke halali wa ndoa. Kauli ya kuomba chumvi inajenga taswira ya tabia ya vijana wengi kujihusisha na mapenzi na wanawake wengi ambao hawana uhalali wa kuwa nao kwani si wake zao. Msanii anasema, chumvi nzuri ni ya kununua na kuifanya yako peke yako, tena mke huyo awe amepewa baraka na wazazi wa pande zote mbili. Hapo utakuwa huru kuitumia namna ambavyo unapenda.

#### 4.2.1.5 Samaki

Samaki ni kiumbe anayeishi ndani ya maji, mwenye mapezi na mkia; viungo ambavyo vinamwezesha kupumua na kwenda ndani ya maji (TUKI, 2015). Kiumbe huyu pia hutumiwa kama kitoweo kwa binadamu wengi. Kwa upande wa lugha ya Kiswahili, samaki amekuwa akitumiwa katika misemo, nahau na methali mbalimbali. Baadhi yake ni; samaki mkunje angali mbichi, samaki mmoja akioza wote wameoza na kilio cha samaki machozi huenda na maji. Kutokana na mifano hiyo, samaki amechorwa katika taswira mbalimbali kulingana na muktadha wa misemo na nahau husika. Msanii Diamond ametumia taswira hii kwenye wimbo wake wa Iyena:

> Imefika tamati,
> Tulisubiri kitambo,
> Leo samaki kanasa kwenye chambo,
> Pongezi kwa kamati,
> Yanavutia mapambo.

Samaki katika mistari hii anaashiria msichana, na sio msichana tu bali ni mke ambaye msanii alikuwa akimtafuta kwa muda mrefu bila mafanikio. Amelinganisha juhudi za kumtafuta huko na shughuli za uvuvi wa samaki kwa kuwarushia chambo. Mara kadhaa amekuwa akikwepa kunasa kwenye mitego yake (chambo), ila wakati

umefika na amenaswa na anafanya harusi kumfanya mke halali wa maisha yake.

Msanii anatumia taswira ya samaki kuonesha thamani ya msichana huyo kwake. Amelinganisha namna samaki anavyochukuliwa katika jamii yetu na kumfanya msichana huyo awe na thamani hiyo. Vilevile, amemtumia samaki kuonesha ni namna gani alikumbana na shida na taabu katika kumpata msichana huyu sawasawa na shughuli za uvuvi wa samaki zilivyo za hatari.

#### 4.2.1.6 Fisi

Fisi ni mnyama wa mwituni anayeaminika kuwa ni mwoga na anayependa kula mizoga. Fasihi ya Kiswahili hususani hadithi, methali kwa kutaja kwa uchache, fisi hutumika kitaswira kumchora mtu mwenye tamaa, mchoyo, mdokozi na mwongo. Msanii Diamond ametumia taswira hii katika wimbo wa Kanyaga:

> Ati kanyaga ka ana pigo za unafiki,
> Kanyaga kama mmbeya asiye rafiki,
> Kanyaga kama fisi ana roho ya usnichi,
> Hakulishi, hakuvishi kwani vipi?

Matumizi ya taswira ya fisi katika wimbo huu yanaakisi muktadha na ujumbe wa wimbo. Wimbo unahusu kuachana na watu wasio na faida katika maisha na kuwatupilia mbali wote wenye mwenendo usiokuwa na faida kwako. Fisi ametumiwa kuonesha watu wenye tabia zinazorandana na tabia za mnyama huyo. Watu wenye tamaa kwenye mafanikio ya watu wengine, unafiki, kutoridhika, wivu usiofaa na uchoyo; wamechorwa katika taswira ya mnyama fisi. Msanii anasema watu wa namna hiyo hawana faida yoyote kwenye maisha yake kwani hawamlishi, kumvalisha wala kumfaa kwa kitu chochote. Uamuzi wa busara ni kuachana na watu wenye mwelekeo unaofanana na tabia za mnyama fisi.

#### 4.2.1.7 Kibakuli cha Vumba

Vumba ni harufu ya samaki na viumbe wengine waishio majini (BAKIZA, 2010). Vumba kwa jina lingine ni shombo (TUKI, 2013). Samaki ni kitoweo chenye thamani kubwa katika jamii ingawa huandamwa na harufu kali (vumba), hasa wakati wa kuandaliwa kwa kitoweo hicho. Harufu hiyo hubaki kwa mwandaaji, chombo cha kusafishia na mahali ilipofanyikia shughuli hiyo.

Neno hili limekuwa likitumika katika lugha ya Kiswahili, hasa kwa watu wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi au kuuza samaki. Msanii Diamond ametumia neno hili katika wimbo wa 'Nasema Nawe':

> Huna haya ka kibakuli cha vumba,
> Popote unajitokeza babueee!
> Haa! we kichoji tu,
> Unaingia kwenye kundi la ninga,
> Utachanika mabawa.

Neno kibakuli cha vumba katika mstari huu limetumika kama taswira kuashiria tabia ya kujipendekeza. Ameambatanishaneno kibakuli cha vumba kuwakilisha chombo kinachotumika kuoshea samaki na hivyo harufu (shombo) ya samaki kubaki kwenye kibakuli hicho. Ili taswira hii ipate maana yake vizuri, ni vyema ikahusishwa na ujumbe wa jumla wa wimbo huu. Taswira hii inachora mtu mwenye tabia ya kujipendekeza na kujipelekapeleka kwa mtu fulani na hiyo kufananishwa na vumba inayobakia kwenye kibakuli baada ya kuosha samaki. Namna ambayo vumba la samaki linavyosambaa kwenye hewa pasipo kuwa na mipaka imelinganishwa na tabia ya mhusika kujitangaza na kujikweza kupita kiasi mbele za watu. Kibakuli ni lugha inayodumaza au kukifanya kidogo sana na kisicho na thamani. Amepewa sifa hiyo kwa namna ambavyo anaonekana. Tabia na mwonekano wake unamfanya aonekane hana thamani na kulinganishwa na kibakuli. Msanii ametumia taswira hii kuwaelezea watu wenye tabia za kujipendekeza na kujionesha mbele za watu wakati hawana thamani hiyo.

#### 4.2.1.8 Ninga

Ninga ni ndege jamii ya njiwa, lakini yeye akiwa ni mkubwa zaidi. Ana rangi ya kijani mwili mzima na miguu myekundu. Hupendelea kuishi juu ya vilele vya miti na kula matunda (TUKI, 2013). Sifa mojawapo ya ndege huyu ni kuwa na uwezo wa kwenda juu zaidi kuliko kundi jingine la njiwa. Hivyo, ana sifa ya kuonekana juu zaidi ya njiwa wengine. Hii inatokana na uwezo wa mabawa aliyoumbwa nayo. Ndege huyu pia ametumiwa kwenye wimbo wa 'Nasema Nawe' kama taswira katika wimbo huo:

> Popote unajitokeza babueee!
> Haa! we kichoji tu,
> Unaingia kwenye kundi la ninga,

Utachanika mabawa.

Mwandishi ametumia taswira hii kuchora kundi la watu wenye tabia za kujikweza au kujipaisha ilhali hali zao sivyo. Kitendo hicho huleta athari katika maisha yao kama ambavyo ndege aina nyingine wanaweza kuchanika mbawa zao wakiwafuata ninga katika vilele vya milima. Hivyo, msanii anashauri watu kuachana na vitu ambavyo hawana uwezo navyo na kuepuka mkumbo. Kuachana na tabia hizo huwaepusha watu kupata madhara mbalimbali kama vile: aibu, magonjwa, madeni na hata kifo. Watu waridhike na kile wanachokipata na kupambana katika njia halali ili kufikia hatua za juu zaidi ili kuweza kutimiza matamanio yao.

Kwa jumla, taswira zilizotumika katika nyimbo za Diamond Platinumz zimeshabihiana na mawazo ya wanasemiotiki kuwa, ishara ni kitu kinachosimama badala ya kitu kingine na kuwa maana zitokanazo na taswira hizi ni mahusiano baina ya kiashiria na kiashiriwa chake.

### 4.2.2 Taswira Zinazojitokeza katika nyimbo za Mrisho Mpoto

Mbali na taswira mbalimbali zilizotumika katika nyimbo teule za Diamond Platnumz, tumebainisha pia taswira katika nyimbo teule za Mrisho Mpoto. Utafiti huu umebaini kuwa nyimbo teule za Mpoto zimetumia taswira mbalimbali zinazohusisha taswira ya mto, ngalawa, mwiba, kuku, chui, roho, nzi, kuni, ugali, nyumba na vyumba.Katika sehemu hii tutafafanua taswira hizo pamoja na maana zake:

#### 4.2.2.1 Mto

Mto ni korongo lenye maji yanayotiririka wakati wote (TUKI, 2013). Msanii Mrisho Mpoto ametumia mto katika wimbo wa ‘Waite.’ Taswira hii imejitokeza katika mstari ufuatao:

Japo mwiba wa kujichoma hauna pole.
Usitenganishwe na mto wakati kuna ngalawa mjomba

Mto ni taswira inayoashiria changamoto au matatizo mbalimbali ambayo husababisha ugumu katika kupata kitu au kufikia kiwango cha juu cha unachokihitaji. Kwa kawaida ili kuvuka mto wowote kunahitajika daraja au kifaa chochote cha kuvukia, ili kufika upande mwingine wa mto. Kama vifaa hivyo

havipo, ni ngumu sana kufika upande mwingine wa mto. Msanii ametumia taswira hii kuashiria matatizo na changamoto zinazowakabili viongozi wengi katika kufikia maamuzi au maendeleo ya jamii zao. Viongozi huelezea sababu kedekede zinazowasababisha wasifikie malengo ya juu katika jamii zao. Msanii anawaasa viongozi kuwa, hawapaswi kukata tamaa wakati kuna ngalawa ndani ya mtu huo. Wanapaswa wapande ngalawa ili wavuke mto huo. Taswira hii pia inajidhihirisha kwenye wimbo wa 'Njoo Uichukue':

> Siku zote naamini mtu huwezi kulala
> kwenye mto hata kama umekauka
> Na ukitaka kujua mwendo wa mjinga
> mpe kilemba uone

Kadhalika, katika mistari hii tunaona taswira ya mto ikitumika kuashiria matatizo au hatari zinazowakabili viongozi mbalimbali. Msanii anawaasa viongozi waache kupuuzia hatari na matatizo yanayozikabili nchi zao kwa kisingizio cha kuwa shida imeisha au imepungua. Amehusianisha na mtu kulala kwenye mto ambao hauna maji, kwa maana mtu hawezi kulala kwenye mto akawa na amani sababu muda wowote maji yanaweza kurudi na kumchukua. Anawataadharisha viongozi kutoridhika na hatua na mbinu wanazochukua kukabiliana na changamoto na hatari hizo.

#### 4.2.2.2 Ngalawa

Ngalawa ni mtumbwi au chombo cha majini chenye kasama iliyofungwa pande zote mbili ili kiwe na uzito sawa, kinachotumiwa katika shughuli za uvuvi (BAKIZA, 2010). Msanii ametumia taswira hii kwenye wimbo wa 'Waite' katika mstari wa ubeti ufuatao:

> Japo mwiba wa kujichoma hauna pole.
> Usitenganishwe na mto wakati kuna ngalawa mjomba

Msanii ametumia taswira ya ngalawa kuashiria kitu au vitu vinavyoweza kutumika kuwavusha watu upande mwingine wa mto. Ngalawa hutumika kusafiria katika mito na bahari, inatumika kubeba vitu mbalimbali kutoka upande mmoja hadi upande mwingine. Anamwambia mjomba, asitenganishwe na mto (matatizo) wakati kuna ngalawa (suluhisho). Picha inayopatikana hapa ni kwa viongozi kuacha kulaumu na kushindwa kufikia malengo yao kwa visingizio vya matatizo mbalimbali. Matatizo

ambayo yanawakabili viongozi wa nchi za Kiafrika kwa kiasi kikubwa zinatatuliwa na vyanzo vilivyopo ndani ya nchi husika. Mfano, matatizo ya umasikini huweza kutatuliwa kwa kutumia rasilimali zilizopo nchini (madini, hifadhi za wanyama na vyanzo vya maji). Rasilimali hizo ambazo zinatumika katika kusuluhisha matatizo hayo (mto) ndio inachora picha ya ngalawa. Kupitia rasilimali hizo, (ngalawa) nchi zetu zinaweza kufikia kiwango cha juu zaidi katika maendeleo. Viongozi waache kulalamika kwa kusingizia matatizo mbalimbali ambayo yanaweza kutatuliwa kwa kutumia rasilimali zilizopo.

#### 4.2.2.3 Mwiba

Mwiba ni sehemu ya mmea yenye ncha inayoweza kuchoma. Pia, mwiba huweza kuwa mfupa wa samaki uliyochongoka au kipande cha sindano au msumari kilichochogoka sana. Neno hili hutumika kwenye lugha ya Kiswahili, hasa kwenye misemo, vitendawili na nahau mathalani, *mdharau mwiba mguu huota tende na aliyechomwa na mwiba, huthamini kiatu*. Maana inayotokana na taswira hizo hutofautiana kulingana na matumizi yake. Mwiba huweza kuashiria kitu chenye kudharauliwa lakini ambacho madhara yake huweza kuwa makubwa zaidi. Mtu anaweza kuchomwa na mwiba kwa bahati mbaya ikiwa atapita sehemu ambayo ina miiba. Msanii ametumia taswira ya mwiba katika wimbo wa 'Waite' katika mstari ufuatao:

Nawashangiliaji wenye sauti zisizo kauka
Japo mwiba wa kujichoma hauna pole
Usitenganishwe na mto wakati kuna ngalawa mjomba

Tunaona msanii ametumia taswira ya mwiba katika hali inayoashiria unyume wa uhalisi wa mambo yalivyo. Kwa kawaida, mwiba humchoma mtu katika mazingira ambayo mtu huyo anakua hajui au hajaona. Mtunzi anasema kuwa mwiba wa kujichoma hauna pole. Katika hali ya kawaida ni vigumu mtu kuchukua mwiba na kujichoma. Kazi za fasihi zina uwezo wa kubadili hali halisi na kuwa kinyume cha uhalisi huo, lengo kubwa likiwa ni katika kufikisha ujumbe kwa walengwa kwa namna iliyo bora zaidi. Taswira tunayopata hapa katika mstari huu ni matatizo mbalimbali ambayo mtu anaweza kukutana nayo kwa kujisababishia, mathalani kwa kuendekeza vitu ambavyo huzalisha matatizo au athari hasi. Msanii anaonesha kuwa

mtu wa namna hiyo hastahili kupewa pole kwa yatakayo mtokea kutokana na matendo yake mwenyewe.

Muktadha wa wimbo huu umeelekezwa zaidi kwa mjomba (kiongozi). Anawaambia viongozi kuwa matatizo mengi (mwiba) yanatokea kwenye uongozi wao ni ya kujitakia (kujichoma). Matatizo kama ya rushwa na ufisadi ni matokeo ya mfumo wa uongozi wenyewe; hayatokani na walio nje ya mfumo huo, hivyo haina haja ya kuwapa pole kutokana na wanayoyatengenza wao wenyewe. Taswira ya mwiba wa kujichoma inawakumbusha viongozi kutafuta vyanzo vya matatizo yanayowakabili kama viongozi na yanayoikabili jamii yao, yanayotokana na makosa yao wenyewe.

#### 4.2.2.4 Kuku

Kuku ni aina ya ndege anayefugwa na binadamu kwa ajili ya kitoweo. Kuku kama walivyo ndege wengine hutaga mayai. Mfugaji anaweza kuyatumia mayai hayo kama chakula, akauza kujiongezea kipato au akaacha kuku ayatamie ili kuongeza kuku wengine. Ndege huyu hutumika katika vitendawili na methali mbalimbali kama vile: *Kuku wangu ametagia mibani* (nanasi), *kuku havunji yai lake* au *dua la kuku halimpati mwewe*. Maana ya taswira hizi hutegemeana na muktadha wa matumizi yake. Mrisho Mpoto ametumia taswira ya kuku katika wimbo wa ‘Sizonje’:

> Kitendawili tega, tega
> Tega nikutege mwiba
> Kuku anayetaga hachinjwi, akichinjwa msiba
> Sizonjeee

Katika wimbo huu, mistari hii, msanii anapomtaja kuku si kwamba anamzungumzia kuku ndege, bali kuku anayetaga ametumika kama taswira inayoelezea shirika linalozalisha na kupata faida katika nchi. Mistari hii ikiunganishwa na mistari mingine ya wimbo huu tunashawishika kuamini kuwa, msanii anatupotumia taswira ya ‘kuku anayetaga hachinjwi, akichinjwa msiba’ inaelezea kuwa mashirika ama taasisi za umma zinazozalisha kwa faida hazitakiwa kuuzwa ama kubinafsishwa kwani kufanya hivyo ni kuua uchumi (msiba) wa taifa.

#### 4.2.2.5 Chui

Chui ni mnyama jamii ya paka anayeishi msituni lakini mkubwa na mkali mwenye madoadoa ya njano na meusi (TUKI, 2013). Miongoni mwa wanyama wakali

msituni, chui ni mmojawapo na ni mnyama wa kuogopwa sana kutokana na kuwa na tabia ya ukatili, ukali na ukorofi wa kila aina, hasa akiwa anatafuta chakula chake. Msanii amemtumia chui kitaswira kwenye wimbo wa ‘Kitendawili’:

Naomba ikumbukwe kwamba,
Aliyemfundisha chui kula watu,
Ni binadamu,
Na anayekunyooshea kidole,
Kuwa naye makini.

Chui ni mnyama ambaye yupo katika kundi la wanyama walao nyama. Chakula hicho hutokana na wanyama wa msituni na wafugwao ila sio nyama ya binadamu. Inasemekana kuwa, chui akionja nyama ya binadamu hunogewa na ni vigumu kuacha kula nyama za binadamu. Katika mistari tunaona msanii anasema, aliyemfundisha chui kula watu ni binadamu. Hapa ametumia tabia na asili ya chui kuihusisha na hali ilivyo kwenye jamii zetu. Taswira ya chui katika mistari hii imetumika kuashiria tabia ya ukatili, ukorofi na ubabe usio na maana. Kimsingi, taswira hii inatupa picha kwamba, matendo ya binadamu wengine ndiyo yanawafanya binadamu wengine wanakuwa wakatili. Watu wa namna hii ni hatari sana kwenye uongozi, kwani huwa ni hatari kwa amani na utulivu wa eneo analoliongoza.

### 4.2.2.6 Roho

Roho ni kitu kisichoonekana, ambacho hufikiriwa kuwa ni sehemu ya mwili wa kiumbe, ambayo hukiwezesha kuwa na uhai (TUKI, 2013). Roho hulinganishwa na kitu cha muhimu kwenye maisha ya binadamu, bila kitu hicho mtu anaweza asione umuhimu wa maisha yake hapa ulimwenguni. Katika fasihi ya Kiswahili, ipo misemo na nahau mbalimbali ambazo huhusisha neno roho. Mfano wa nahau ni kama vile; *kata roho* (kufariki), *kaza roho* (vumilia) na msemo *roho mkononi* (kuwa na wasiwasi). Msanii ametumia taswira ya roho kwenye wimbo wa ‘Njoo Uichukue’:

Eeeh eeh
Roho yangu kama itakusaidia (ndugu yangu)
Kama itakupa ushindi
Moyo wako najua
Kama itakusaidia kama itakupa ushindi moyo wako najua
Usiku rafiki wa giza

Basi njoo uichukue×3

Muktadha wa wimbo huu ni wa kisiasa, hasa katika harakati za kampeni na uchaguzi wa viongozi. Mazungumzo baina ya mgombea na mwananchi katika harakati za kuhitaji nafasi ya kuwa kiongozi. Roho imetumika kuashiria kura. Kura ni kitu muhimu katika kufanya maamuzi ya viongozi wa jamii yoyote. Thamani ya kura ya mtu mmoja inaweza kubadilisha matokeo ya uchaguzi. Msanii amelinganisha thamani ya kura kuwa ni sawa na thamani ya roho ya kiumbe hai. Wananchi wanatakiwa wafahamu umuhimu wa kura zao katika kuzifanya jamii zao kuwa na maendeleo, na hivyo kuacha utaratibu wa kuuza kura zao kwa nguo au fedha. Mazungumzo ya wimbo huu yanaashiria matatizo ambayo wananchi wanakabiliana nayo katika jamii zao. Matatizo haya yanadhihirika kwa msanii kumwambia mgombea afuate kura kule zilipo ili apate kufahamu matatizo yao. Katika wimbo huu, roho ni taswira ya kura ambayo msanii anaamini ndiyo roho ya maendeleo ya jamii na hivyo inatakiwa kutumiwa vizuri.

#### 4.2.2.7 Nzi

Nzi ni mdudu mdogo anayeruka na anayependa kukaa mahala pachafu na hueneza magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu (BAKIZA, 2010). Sifa kubwa ya mdudu huyu ni uchafu. Tabia ya kushinda kwenye vitu vilivyoharibika na kuoza ndio makazi yake. Nzi hutupa taswira ya uchafu inapotumika katika mazungumzo ya kawaida. Mdudu huyu pia hutumika katika misemo mbalimbali kama: *penye uchafu hapakosi nzi* au *nzi hufia kwenye kidonda*. Msanii ametumia taswira ya nzi katika wimbo wa ‘Njoo Uichukue’:

Nakukumbusha ukitaka nzi wasikufute,
Acha kula vilivyooza,
Chuki humchoma aliyehifadhi,
Kwenye moyo siku zote.

Taswira inayojitokeza kutokana na neno nzi kwenye mstari huu ni uchafu ambao unahusishwa na viongozi ambao hufanya mambo yasiyofaa. Mambo hayo ni pamoja na dhuluma za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni zinazofanywa na viongozi wa jamii yetu. Viongozi ambao hupendelea na kuendeleza mambo hayo, wamechorwa kama nzi katika wimbo huu. Kiongozi akitaka kuacha tabia ya nzi ni

lazima ajiweke katika mazingira yaliyo safi. Msanii anawahusia wagombea wanaoomba ridhaa ya kuongoza wakitaka kuwa safi ni lazima wajitenge na uchafu wa namna zote wakipata nafasi hizo.

#### 4.2.2.8 Kuni

Kuni ni vipande vya mti vinavyotumika kukokea moto. Zinaweza kuwa mbichi au kavu kulingana na mahitaji ya mhusika. Kuni kavu hutumika katika matumizi ya kila siku kama vile: kupikia, wakati kuni mbichi kwa kiasi kikubwa hutumika katika kutengenezea mkaa. Kuni mbichi zikitumika katika shughuli za upishi huleta shida na matatizo katika upishi tofauti na kuni kavu. Mrisho Mpoto ametumia taswira ya kuni katika wimbo wake wa ‘Chocheeni Kuni’:

> Hey, yea ooh,
> Chocheeni kuni mbichi,
> Moto ukoleee, ugali uive,
> Mnacho taka kitokee

Taswira ya kuni katika wimbo huu imetumika kuashiria sera au mipango ya nchi ili kupata maendeleo zaidi. Msanii anatumia taswira yenye kejeli ndani yake kwa viongozi kwa njia wanazotumia kufikia maendeleo hayo. Kuni mbichi zimeashiria sera au mipango ambayo ni migumu kutekelezeka, na hivyo kukwamisha kufikia maendeleo (kuiva kwa ugali). Ujumbe unaopatikana kutokana na taswira hii ni kwa viongozi kuandaa sera ambazo ni rafiki kwa wananchi na ambazo zinatekelezeka.

#### 4.2.2.9 Ugali

Ugali ni chakula kinachopikwa kwa unga wa mahindi au mtama kwa kusongwa (TUKI, 2013). Ni aina ya chakula ambacho kinatumiwa katika jamii nyingi za Kiafrika. Ili kupata ugali mzuri, lazima kuwe na maandalizi mazuri kabla na wakati wa kupika. Mfano: maandalizi ya nafaka, unga na mpishi ni vitu vya muhimu. Msanii anapozungumzia ugali katika wimbo wa ‘Chocheeni Kuni’ si kwamba anazungumzia ugali akimaanisha chakula. Hii ni taswira inayoelezea maendeleo au mafanikio. Rejelea wimbo tajwa msanii anaposema hasa katika kiitikio:

> Chocheeni kuni mbichi moto ukolee,
> Ugali uive mnachotaka kitokee,
> Alikeni mamluki, wakija wangojee,

Mikeka waweke, mnachotaka kitokee.

Hapa msanii anawakejeli viongozi, anawaona wanatumia kuni mbichi kuchochea moto ili waivishe ugali. Hii ni kejeli ambayo imetumika kitaswira. Taswira ya kuni mbichi ni mipango mibovu wakati taswira ya ugali inahusianishwa na kupatikana kwa maendeleo au mafanikio. Kwa mantiki hii, taswira ya ugali kama tulivyodokeza awali ni taswira inayohusu maendeleo ama mafanikio.

### 4.2.2.10 Nyumba

Nyumba ni jengo ambalo limeandaliwa kwa ajili ya mtu au watu kuishi. Taswira ya nyumba hutumika katika lugha ya Kiswahili kuashiria vitu mbalimbali kulingana na muktadha wa matumizi yake. Taswira hii tunaikuta katika vitendawili, mfano, 'nyumba yangu ndogo (kiberiti), nyumba yangu haina mlango (yai)'. Matumizi ya taswira hutegemeana na mahali na kusudio la matumizi yake. Mrisho Mpoto ametumia taswira ya nyumba katika wimbo wa 'Sizonje':

Sizonje hii ndio **nyumba** yetu
Milango ipo wanapita madirishani
Sizonje ndio nyumba yetu milango ipo
Wanapita madirishani
Ingia uyaone, maajabu ya nyumba yetu

Taswira ya nyumba katika wimbo huu imetumika kuchora serikali ya taifa au nchi. Muktadha wa wimbo huu ni wa kisiasa na unahusiana na kumkaribisha kiongozi kwenye madaraka baada ya kuchaguliwa kuongoza serikali ya taifa au nchi. Msanii anamwelezea jinsi nyumba (serikali) ilivyo na ajiandae kuiongoza katika namna ambayo ataona itafaa. Anamwelezea tabia ya serikali ya nchi na taifa lake ilivyo. Nyumba ambayo imetawaliwa na maajabu mbalimbali ndani yake hivyo awe makini katika kufanya yale aliyoyakusudia kuyafanya.

### 4.2.2.11 Vyumba

Vyumba ni sehemu zilizogawanywa ndani ya nyumba moja. Hutumika kwa matumizi mbalimbali kama vile: kulala, sebule na jiko. Wimbo wa 'Sizonje' umetumia taswira ya vyumba katika beti zake kwa kueleza sifa ya kila chumba:

Nyumba hii Sizonje ina**vyumba** vinne,

Vitatu havifunguki, kimoja hakina mlango,
Japokuwa kina watu ndani, na hawaongei Kiswahili,
Wenyeji wanalala sebuleni na walishazoea,
Sizonje kule tulipotoka panaitwa jikoni

Muktadha wa wimbo huu umekitwa katika mwelekeo wa kisiasa, hasa siasa ya nchi ya Tanzania. Kama tulivyoona hapo juu kuwa taswira ya nyumba ni serikali, kulingana na taswira hiyo, tunapata picha kuwa, vyumba anavyovizungumzia msanii ni awamu za uongozi zilizopita. Tanzania imepitia katika awamu nne za uongozi na sasa tupo awamu ya tano ya utawala. Anaelezea namna nyumba ambayo ameingia ilivyo na jinsi serikali zake zilivyo. Tunaweza kusema kuwa awamu ya kwanza hadi ya tatu ndio vyumba vilivyofungwa (mambo yaliyofanyika katika awamu hizo hayajadiliwi wala kuzungumziwa). Chumba cha nne kilichowazi, ni awamu ya nne ambayo nayo ndio ilikuwa imemaliza kipindi chake. Mambo ya chumba hichi hujadiliwa na kuzungumziwa kwa uwazi na kiasi kikubwa.

Taswira hii inatupa ufahamu kuhusiana na jinsi mambo yanavyoendelea katika serikali zetu, msanii anampitisha Sizonje katika nyumba hiyo na kumwonesha udhaifu na matatizo ya nyumba hiyo. Namna taswira zilivyotumika katika nyimbo za Mrisho Mpoto zinadhihirisha mawazo ya wanasemiotiki kuwa, taswira ambazo zimetumika zina uhusiano na viashiriwa vyake. Kupitia uhusiano huo, maana ya taswira hizo zimepatikana na hivyo wimbo huu kueleweka kwa hadhira yake.

### 4.3 Dhima ya Taswira katika Nyimbo za Waimbaji Teule

Sanaa huwa na dhima mbalimbali katika jamii kusudiwa. Dhima hizo huweza kushabihiana ama kutokushabihiana kutoka jamii moja hadi jamii nyingine. Utumiaji wa taswira katika nyimbo za wasanii huwa na dhima mbalimbali. Dhima hizo hufanana na kutofautiana kutoka kwa msanii mmoja hadi mwingine. Miongoni mwa dhima zilizobainika ni pamoja na kukwepa udhibiti, kufikisha ujumbe, kuonesha ufundi wa msanii, kuvutia hadhira, kuburudisha hadhira na kupamba kazi za msanii. Sehemu hii inabainisha dhima za taswira kama zilivyotumika katika nyimbo zetu teule kama ifuatavyo:

#### 4.3.1 Kukwepa Udhibiti

Mwanzoni mwa miaka ya 1990, muziki wa kizazi kipya ulikuwa ukipingwa vikali na jamii kutokana na kuzungumzia mambo kwa uwazi hasa yanayohamasisha

mahusiano ya kingono, ulevi wa pombe, madawa ya kulevya na vurugu. Hali kadhalika ulionekana kuwa ni muziki unaotumia lugha ya matusi. Mambo haya kwa ujumla wake yalisababisha muziki huu kudhibitiwa katika vyombo vya habari. Katika jitihada za kukwepa udhibiti wa aina hii, pamoja na mambo mengine, wasanii wakabadilika na kuanza kutumia lugha ya taswira/picha kuzungumzia mambo yaleyale ili kazi zao zisiweze kudhibitiwa. Matumizi ya taswira yanawapa uhuru zaidi wasanii kuzungumzia mambo mbalimbali katika tungo zao bila kuhofia udhibiti wa dola au jamii[2].

Katika wimbo wa ‘Salome’ tunaona namna ambavyo Diamond ameweza kutumia taswira kupunguza ukali wa maneno halisi. Mfano katika mistari hii:

> Iyo michezo ya jongoo
> Mbona watizama chini Salome wangu
> Ukimuona **jongoo**
> Inama kidogo, shika magoti
> Mimi nimesimama kama **ngongoti**.

Hapa msanii ametumia taswira za jongoo na ngongoti kuashiria sehemu za uzazi za mwanaume, matumizi taswira hizi kumeifanya nyimbo hii kukwepa mkono wa dola. Vilevile, tunaona namna ambavyo msanii Mrisho Mpoto anavyozungumzia siasa katika lugha ya taswira na kumwezesha kuukwepa nguvu za dola katika nyimbo zake. Mdhihiriko mzuri ni majina ya wahusika wake katika nyimbo zake, majina kama ‘Sizonje’ na ‘Mjomba’ yanatumika kiishara tu kuwakilisha viongozi wakubwa katika nchi ya Tanzania. Hivyo, kwa kiasi kikubwa utumiaji wa taswira huwawezesha wasanii mbalimbali kuzungumza kwa uhuru na kukwepa udhibiti wa kazi hizo na nguvu ya dola.

Pamoja na matumizi ya taswira kudhibiti kufungiwa kwa kazi za wasanii, baadhi ya wasanii hutumia taswira za wazi kabisa na kuishia mikononi mwa sheria (BASATA). Sheria hizo ni pamoja na kusimamishwa kwa muda kujishughulisha na sanaa au kufungiwa kwa nyimbo husika. Baadhi ya nyimbo ambazo zimekumbana na kufungiwa kutokana na uwazi wa taswira ni: 'Mwanza' (Rayvanny na Diamond); 'Nampa Papa' (Gigi Money); 'Kibamia' (Rostam); 'Bongo Bahati' Mbaya (Young D);

[2]Maelezo haya yametolewa na DJ Soliso. DJ Soliso anafanya kazi zake Temeke, Dar es Salaam. Alitoa maelezo haya alipofanya mazungumzo na mtafiti tarehe 10.04.2020.

kwa kuzitaja kwa uchache tu, hizi ni miongoni mwa nyimbo zilizofungiwa na BASATA kutokana na kuonekana kwamba hazina maadili licha ya nyimbo hizi kutumia taswira.

### 4.3.2 Kufikisha Ujumbe

Lugha ndiyo nyenzo kuu katika kazi ya fasihi inayotumika kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa na msanii. Tasinifu hii imebaini kuwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya hutumia taswira kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii. Ujumbe wa msanii ndio humshawishi atumie taswira ya namna gani katika kuifikia hadhira. Nyimbo teule ambazo zimejengwa kwa taswira zimedhihirisha hoja hii kwa kina zaidi. Wimbo wa Mrisho Mpoto wa 'Njoo Uichukue' unawasilisha ujumbe wa kisiasa kwa kuelezea namna ambavyo viongozi wanavyopaswa kufanya katika kutatua changamoto za wananchi wao. Mfano katika mistari ifuatayo:

> Siku zote naamin mtu hawezi kulala
> kwenye mto hata kama umekauka
> Na ukitaka kujua mwendo wa mjinga
> mpe kilemba uone.

Msanii ametumia taswira ya mto kuonesha hatari iliyopo kama viongozi wakiridhika na hatua ndogo walizochukua katika kutatua matatizo ya wananchi wao. Halikadhalika katika nyimbo nyingine amewasilisha ujumbe unaoegemea zaidi kwenye siasa na kuwakumbusha viongozi kuwajali, kuachana na dhuluma na uonevu. Msanii Diamond Platinumz kwa kiasi kikubwa taswira katika nyimbo zake zimejikita kufikisha ujumbe wa kimapenzi. Tunaona namna ambavyo taswira inatumika kufikisha ujumbe katika namna ambayo inahitaji uelewa wa kina zaidi. Mfano katika wimbo wa Salome:

> Mimi nimesimama kama ngongoti
> Mtoto jojo, sio roboti
> Chumbani bingilibingili sambasoti.

Taswira hii imetumika kuonesha namna ambavyo wahusika wawili (wapenzi) wanavyohitajiana kingono pasipo kutaja viungo kwa lugha ya uwazi. Namna ambavyo mwanamke anamfanya mwanaume ajisikie raha wakiwa katika tendo hilo linalozungumziwa katika lugha ya taswira pia.

Pamoja na ukweli kwamba taswira hutumika kuwasilisha ujumbe wa msanii, tasinifu hii imebaini kuwa wasanii wengi wanatumia taswira katika kufikisha ujumbe wao. Changamoto kubwa inakuwa katika upokelewaji wa taswira hizo kwa hadhira husika. Baadhi hupokelewa katika mtazamo hasi na kusababisha kazi hizo kufungiwa na kulipishwa faini. Baadhi ya taswira hushawishi watu kujiingiza katika matendo yasioyofaa, kama vile: mapenzi kinyume cha maumbile, matumizi ya madawa ya kulevya, ulevi na umalaya.

Ujumbe unaopatikana kutokana na matumizi ya taswira, hurejelea mawazo ya nadharia ya semiotiki kuwa, jambo lolote litakuwa na maana iwapo litatafsiriwa kwa kurejelewa. Urejezi huo hufanyika kulingana na maisha halisi ya hadhira lengwa.

### 4.3.3 Kuonesha Ufundi wa Msanii

Tasinifu hii imebaini kuwa baadhi ya wasanii wa muziki wa kizazi kipya hutumia taswira kwa lengo la kuonesha ufundi wao wa matumizi ya lugha katika kusana kazi zao. Matumizi ya taswira huwapa wasanii sifa ya kuonekana watunzi wazuri wa mashairi na wajuvi wa kutumia lugha katika kazi zao. Ubora wa msanii huonekana katika matumizi ya lugha katika kuwasilisha ujumbe wake kwa jamii[3]. Sifa za namna hii ndiyo huwasukuma wasanii wengi kuamua kutumia taswira katika tungo zao. Namna ambavyo msanii Mrisho Mpoto anatumia taswira katika nyimbo zake hudhihirisha ufundi na usanii wa kiwango cha juu. Matumizi ya taswira ambazo huwaacha hadhira katika mielekeo tofauti ya maana zake. Mfano katika wimbo wa ‘Kitendawili’:

> Ndugu zangu, inawezekana kweli tumechoka maharage
> Lakini kama tunataka nyama tusubirini kwanza banda lijae.

Katika mistari hii tunaona namna ambavyo msanii ametumia taswira ya maharage na nyama kufikisha ujumbe muhimu kwa wananchi na viongozi kwa ujumla kwa lugha yenye ufundi. Vilevile, anawashauri viongozi kuwa wastahimilivu ili kufikia maendeleo ya kiwango cha juu kuliko kupitia njia fupi za kufikia maendeleo hayo. Utumiaji wa taswira ni mbinu ambayo humtofautisha msanii mmoja na mwingine katika kuonesha ufundi wa kutumia lugha.

[3]Maelezo haya yametolewa na Bw. Yohana Sasi. Yohana Sasi ni mkazi wa Ubungo, Dar es Salaam. Maelezo haya aliyatoa tarehe 21/03/2020 alipofanya mahojiano na mtafiti.

### 4.3.4 Kuvutia Hadhira

Hii ni dhima nyingine inayowasukuma wasanii kutumia taswira katika kazi zao. Tasinifu hii inaonesha kuwa, wasikilizaji wengi wa muziki wa kizazi kipya wanavutiwa sana na matumizi ya taswira kutokana na uwezo wa taswira hizo kuibua hisia mbalimbali za msikilizaji. Aidha, tasinifu hii imebaini kuwa nyimbo nyingi za wasanii wa muziki wa kizazi kipya huwa na taswira zinazoweza kumfanya msikilizaji kuona, kugusa, kunusa, na kuonja ladha ya kinachozungumziwa na kisha akapata msisimko kutokana na aina ya taswira zinazobebwa katika tungo husika. Taswira za aina hii ndizo huwavutia wasikilizaji kupenda tungo za muziki huu. Mfano katika wimbo wa 'Sizonje' tunaona namna ambavyo mtunzi ameweza kuivuta hadhira kwa kutumia mhusika wa kitaswira:

> Sizonje hii ndio nyumba yetu
> Milango ipo wanapita madirishani
> Sizonje hii ndio nyumba yetu
> Milango ipo wanapita madirishani
> Ingia uyaone, maajabu ya nyumba yetu.

Matumizi ya taswira ya Sizonje yanaivuta hadhira kwa karibu na kuibua hisia za kutaka kufahamu Sizonje wa kweli ni nani na ni nini kusudio la mtunzi kutumia taswira hiyo. Kwa jumla, baadhi ya taswira huishawishi hadhira katika kufuatilia tungo za msanii husika, matumizi mazuri ya lugha na taswira huwezesha tungo ya msanii kupokelewa vizuri.

### 4.3.5 Kuburudisha Hadhira

Wasanii wa muziki wa kizazi kipya wakati mwingine huamua kutumia taswira kwa lengo la kuburudisha wasikilizaji wao[4]. Tasinifu imebaini kuwa zipo nyimbo za muziki wa kizazi kipya ambazo zinabeba taswira ambazo dhima yake kubwa ni kuburudisha, kufurahisha na kuchekesha jamii kama sehemu ya kuiliwaza na kufurahia wanaposikiliza nyimbo husika. Taswira za aina hii mara nyingi huwa hazina ujumbe mahususi kwa jamii zaidi ya kuburudisha. Mfano mzuri tunaona katika wimbo wa 'Kanyaga' wa Diamond Platinumz:

[4] Maelezo haya yametolewa na Bi. Magreth Shirima. Magreth ni mwanafunzi wa mwaka wa pili wa shahada ya kwanza katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma. Maelezo haya aliyatoa tarehe 21/02/2020.

Kanyaga!
Uzushi, Kanyaga!
Mashemu feki, Kanyaga!
Nuksi, Kanyaga!
Kudadadeki, Kanyaga!
Mawifi, Kanyaga!
Mpaka ma ex, Kanyaga!
Mikosi, Kanyaga!
Woooya Kanyaga

Pamoja na ujumbe unaotokana na taswira ya kanyaga katika wimbo huu, lengo jingine kubwa la taswira hii ni kuburudisha wasikilizaji wa wimbo huu. Taswira hutoa burudani katika masikio ya wasikilizaji wake na kufanya kazi ya msanii huyo kupendwa na kukubaliwa zaidi. Namna wimbo huu ulivyopokelewa na hadhira inadhihirisha namna ambavyo taswira ya kanyaga ilivyowavutia na kuwaburudisha.

### 4.3.6 Kupamba Kazi za Msanii

Wasanii wa muziki hutumia taswira katika kuzifanya kazi zao kuvutia na kupendeza kwa wapokeaji wa kazi hizo. Taswira huzipa kazi za wasanii sura ya kupendeza na kuvutia masikioni mwa wasikilizaji wake. Aidha, tasinifu hii imeonesha namna ambavyo wasikilizaji wanapenda na kufurahia matumizi ya taswira katika muziki wa kizazi kipya[5]. Mfano wa matumizi mazuri ya taswira katika kupamba kazi za wasanii umedhihirika zaidi katika tungo za Mrisho Mpoto:

Unawaulizaje Watu magongo ya nini?
Wakati Umesema kuna nyoka!
Mjomba, wewe si uliwapaka wanja,
Ngoja wao wakupake pilipili,
Halafu kwenye kombolela iwe zamu yako kuzinga

Wimbo huu wa ‘Njoo Uichukue’ umedhihirisha namna ambavyo mtunzi ametumia taswira katika kupamba kazi yake. Taswira kama magongo, nyoka, mjomba, wanja na pilipili zimetumika kuongeza ubora wa kazi ya msanii na kupamba lugha ya Kiswahili katika kufikisha ujumbe kusudiwa. Matumizi ya taswira huifanya hadhira kufikiria kwa makini ili kupata ujumbe unaobebwa na taswira husika.

[5]Maelezo haya yametolewa na Bw. Yusufu Shitenge, kijana mkazi wa Dodoma. Mazungumzo yaliyofanyika eneo la Makulu siku ya tarehe 02/04/2020 alipofanya mahojiano na mtafiti.

### 4.4 Athari za Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Waimbaji Teule

Matumizi ya taswira katika kazi za fasihi huambatana na athari mbalimbali kwa hadhira yake. Athari hizo huweza kuwa hasi au chanya. Tasinifu hii imegawa athari za matumizi ya taswira katika nyimbo za waimbaji teule katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni athari chanya wakati sehemu ya pili ni athari hasi.

#### 4.4.1 Athari Chanya za Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Waimbaji Teule

Utafiti huu umebaini kuwa matumizi ya taswira katika nyimbo teule una athari mbalimbali chanya. Athari hizo ni chanya kwa kuwa zinaboresha na kufanya kazi za wasanii hao kuwa na mapokeo mazuri kwa hadhira. Miongoni mwa athari chanya za matumizi ya taswira katika nyimbo teule ni pamoja na kuibua hisia za hadhira/wasikilizaji, hukuza udadisi wa hadhira, huchochea kupendwa na kukua kwa kipera husika, hufanya maudhui yaeleweka kwa urahisi na kudumisha maadili ya jamii.

##### 4.4.1.1 Huibua Hisia za Hadhira/Wasikilizaji

Wasanii wa kazi za fasihi wakiwemo wasanii wa muziki wa kizazi kipya hutumia taswira kwa lengo la kuibua hisia mbalimbali za wasikilizaji wao. Kutokana na aina ya taswira zitumikazo, msikilizaji anaweza pata hisia za mguso, uoni, ladha au mnuso. Ieleweke kwamba, msikilizaji anaweza pata hisia za namna hii kutokana na uwezo wake wa kuzitafsiri taswira husika na ufundi wa msanii katika kuziumba taswira hizo. Mfano wa hisia inayotokana na matumizi mazuri ya taswira inajidhihirisha katika wimbo wa ‘Njoo Uichukue’ katika mistari ifuatayo:

> Alama kubwa utakazokutana nazo ni visheti na chipsi dume,
> Kashata na maandazi, chapati na uroge wa ubuyu,
> Pweza na vijiti vyake
> Ukiona sufuria la supu unakaribia
> Maana nchi yenu nchi yetu pia
> Hapa watu pale kinyesi na kondomu ndo kwetu
> Dampo dogo pale pembeni maji ya mtungi nyumbani huko
> Chumba cha baba hapa choo cha pipa pembeni
> Unakaribia

Hisia inayotokana na matumizi ya taswira kadhaa katika mistari hii inathibitisha mazingira machafu na hali ngumu za wakazi wa eneo husika. Mtunzi ametumia

taswira za hali hiyo kuashiria hali ngumu zilivyowazunguka watu wa tabaka la chini. Hisia za kinyaa, kuchefua na kukarahisha, hudhihirika kupitia mpangilio wa taswira hizo. Ufundi wa kuchora taswira katika kazi za sanaa huchangia katika kuibua hisia mbalimbali kwa hadhira lengwa.

### 4.4.1.2 Hukuza Udadisi wa Hadhira

Kwa hakika kazi mojawapo ya msanii wa kazi ya fasihi ni kuchochea na kukuza udadisi wa hadhira yake. Taswira zinazotumika katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya pia huibua na kukuza udadisi miongoni mwa wasikilizaji wake. Pengine swali laweza kuwa ni kwa namna gani msikilizaji anaweza pata athari hii? Taswira ni lugha ambayo maana yake huwa si ya wazi, hali inayomfanya msikilizaji kutafuta kwa kina maana ya taswira husika ili kujua msanii anamaanisha nini? Kwa kufanya hivi msikilizaji hujikuta akikuza uwezo wake wa kudadisi wa kazi za fasihi. Taswira za namna hii zinajidhihirisha zaidi katika nyimbo za Mrisho Mpoto. Katika wimbo wa ‘Sizonje’ tunaona namna anavyotumia taswira katika kukuza udadisi kwa hadhira kutaka kufahamu zaidi kuhusiana na kilichofichwa ndani yake:

> Najua, wimbo mbaya haufai kubembelezea mtoto
> Na kamwe mtoto hawezi kuungua
> Kwa kiazi kilichokuwa kwenye kiganja cha mama yake mzazi
> Njoo huku uone, Sizonje si unajua,
> harufu ya uzazi haiishi mpaka mtoto akue.

Udadisi wa hadhira hukuzwa na matumizi ya taswira ambayo huchochea fikra zao kufikiri na kutafuta kuhusiana na taswira husika. Mfano katika mistari hii tunaona taswira zenye kuamsha ari ya udadisi kwa hadhira kwa kutafuta maana ya misemo iliyotumika katika mistari ya wimbo huu. Nafasi kubwa ya wasanii kutumia taswira imewekwa katika kuamsha ari na kuwafikirisha ili kupata maana iliyokusudiwa na mtunzi wa wimbo.

### 4.4.1.3 Huchochea Kupendwa na Kukua kwa Kipera Husika

Wasikilizaji wa muziki wa kizazi kipya huvutiwa sana na nyimbo ambazo zina ufundi wa matumizi ya lugha ikiwa ni pamoja na matumizi ya taswira. Wakati mwingine wimbo unaweza usipendwe kwa mara ya kwanza unaposikilizwa endapo

utakuwa na taswira zenye uhitaji wa kufikiria zaidi[6]. Wimbo huonekana kupendwa na kufuatiliwa pale taswira zinapokuwa zimeeleweka kwa wasikilizaji wake. Wasikilizaji wengi hudai kwamba nyimbo zilizojaa taswira hupendwa kutokana na ukweli kwamba leo wanaweza pata ujumbe fulani, kesho wakapata ujumbe mwingine katika wimbo huo huo.

Kipera cha muziki wa kizazi kipya hupendwa na hadhira yake kutokana na matumizi ya taswira katika kufikisha ujumbe wake. Wasanii hutumia taswira ili kuifikia hadhira lengwa na kufanya aina ya muziki huu kukimbiliwa na vijana wengi katika kujipatia kipato cha kila siku. Vilevile, matumizi ya taswira huchochea kuendelea kukua kwa kipera hiki. Hali ya kutumika sana katika jamii hufanya aina hii ya muziki kuendelea kuishi na kuimarika kwa utanzu huu.

### 4.4.1.4 Hufanya Maudhui Yaeleweke kwa Urahisi

Tasinifu hii imebaini kuwa, taswira huweza kusaidia ujumbe wa msanii wa tungo za muziki wa kizazi kipya kuweza kueleweka kwa urahisi. Hii ni kwa sababu msanii anaweza kueleza jambo kwa upana na urahisi kwa kutumia taswira. Halikadhalika, tasinifu imebaini nyimbo za wasanii wa muziki huu hutumia taswira zinazoibua hisia mbalimbali, hisia zinazoweza kumrahisisishia msikilizaji kuelewa kwa urahisi ujumbe uliomo katika wimbo husika. Katika wimbo wa ‘Sizonje’ wa Mrisho Mpoto tunaona namna ambavyo umetumia taswira ya bahasha za khaki kuashiria tatizo kubwa la ajira kwa vijana wa leo. Wimbi hilo linaongezeka siku hadi siku kulingana na wahitimu wa vyuo mbalimbali kukosa ajira za kudumu. Tunaiona taswira hiyo katika mistari ifuatayo:

> Kama ukiwa makini kwa nje utasikia sauti za makundi ya watu
> Wengi ni vijana, wana bahasha za khaki mikononi

Hata hivyo, kueleweka kwa urahisi kwa maudhui yabebwayo na taswira, hutegemea kwa kiasi kikubwa uwezo wa msikilizaji katika kuijua lugha iliyotumika na utamaduni wake. Pia uwezo wa kuhusisha vidokezo au viashiria vibebwavyo na taswira husika katika tungo kwa kuhusianisha na ulimwengu halisi unaomzunguka. Kinyume cha uwezo huu itakuwa ni vigumu kwa msikilizaji kuuelewa kwa urahisi

[6]Maelezo haya yametolewa na Bi. Peace Manyilizu. Peace ni kijana anayeishi Chanika, Dar es Salaam. Alitoa maelezo haya alipofanya mazungumzo na mtafiti tarehe 16/03/2020.

ujumbe kusudiwa.

#### 4.4.1.5 Hudumisha Maadili ya Jamii

Kwa hakika katika matumizi ya lugha kila jamii huwa na maadili yanayopaswa kuzingatiwa na watumiaji wa lugha husika. Yapo maneno ambayo kutokana maadili ya jamii hayawezi kutamkwa hadharani, hasa maneno yanayotaja sehemu za siri. Baadhi ya wasanii wa muziki wa kizazi kipya wanaonekana kuzingatia maadili ya jamii kwa kuepuka kutumia manene makali na badala yake hutumia taswira kwa kupunguza ukali wa maneno husika. Mfano wa maneno hayo ambayo hupunguza ukali wa maneno ni kama vile, jongoo (uume) katika wimbo wa 'Salome' (Diamond na Rayvanny), Katika wimbo wa ‘Iyena’ tunaona namna ambavyo msanii anatumia taswira kuhimiza kufuata miiko na maadili ya jamii iliyopo. Tunaona hilo katika mistari ifuatayo:

> Ahsante mama ulinifunza nkajua
> Baba kasema kuomba mwiko
> Raha ya chumvi kununua
> Tena si kwa nazi
> Si hirizi za waganga
> Kwa baraka za baba na mama
> Tu na dua.

Ujumbe unaoashiriwa na taswira ya chumvi katika wimbo huu ni moja ya maadili ya jamii za Kiafrika. Chumvi imetumika kuashiria mke katika wimbo huu. Msanii anaelezea namna njema ambayo inafaa kufuatwa na wanajamii (wanaume) ili kuanzisha familia. Familia njema inaanzishwa kwa makubaliano na baraka toka kwa wazazi husika. Ujumbe unaotolewa hapa unalingana na hali halisi katika jamii yetu, vijana wanakutana na kuanzisha tu familia pasipo kuwa na baraka au ruksa toka kwa wazazi. Moja ya miiko na maadili ya jamii zetu ni kuzingatia maadili hayo.

### 4.4.2 Athari Hasi za Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya

Mbali na athari chanya, tumebaini kuwa, matumizi ya taswira pia yana athari hasi. Athari hizi ni zile ambazo zinaaathiri uwasilishaji na mapokezi ya kazi husika za fasihi. Miongoni mwa athari zilizobainika ni pamoja na kusababisha ugumu katika kupata undani wa maudhui yanayokusudiwa, kuchochea mmomonyoko wa maadili na pia kusababisha utata wa maana

#### 4.4.2.1 Husababisha Ugumu wa Kupata Undani wa MaudhuiYanayokusudiwa

Taswira ni lugha ya mafumbo ambayo wakati mwingine hutumika ili kuficha jambo linalozungumziwa kuwa la siri[7] kwa maana ya kutofahamika na watu wengine wasiohusika. Tasinifu imebaini kuwa, wasikilizaji wengi hawaelewi vizuri maana ya taswira zitumikazo katika nyimbo hizo, hivyo kushindwa kuelewa undani wa maudhui yayobebwa na taswira hizo. Miongoni mwa wasikilizaji hufikiri kwamba wasanii hutumia taswira kwa lengo la kupamba kazi zao tu na kushindwa kuzingatia maudhi yanayobebwa na taswira hizo. Katika wimbo wa 'Sizonje' tunaona namna ambavyo mtunzi ametumia lugha ya taswira kufikisha ujumbe ambao ni vigumu kueleweka:

> Sawa Sizonje, huu hapa ni **ua**
> Lile pale ni **shimo la taka**, na kile pale ni **choo**
> Kinachotutisha na kutuogopesha zaidi
> Wanaoishi humu ndani hawajawahi kutupa taka wala kwenda chooni

Taswira kama ua, choo na shimo la taka zimetumika kuonesha tatizo kubwa la ajira linalowakumba vijana wa kipindi cha sasa. Kuelewa maana ya taswira hizi kunahitaji weledi mkubwa wa lugha kwa wasikilizaji wake. Wasikilizaji wasipoweza kutumia ujuzi wa lugha huishia kuona taswira zimetumika katika kupamba lugha na kupendezesha utanzu husika. Hivyo ujumbe lengwa unaachwa na kutokumakinikiwa na hadhira na wahusika.

#### 4.4.2.2 Huchochea Mmomonyoko wa Maadili

Zipo nyimbo za muziki wa kizazi kipya ambazo zina taswira, hasa za mapenzi zinazochochea mmomonyoko wa maadili katika jamii. Nyimbo za muziki wa kizazi kipya hupendwa sana na vijana na watoto[8]. Huziimba na wakati mwingine huamua kutenda yale yanayoimbwa na wasanii wanaowapenda. Mfano wa taswira ambazo huchochea matendo yasiyo na maadili kwa jamii imejidhihirisha katika wimbo wa Diamond Platinumuz wa 'Salome':

> Inama kidogo, shika magoti

[7]Maelezo hayo yametolewa na Bw. John Magway. John ni kijana wa miaka 24 na mkazi wa Makulu, Dodoma. Maelezo haya aliyatoa alipofanya mahojiano na mtafiti tarehe 05/04/2020.
[8]Maelezo haya yametolewa na Bw. Castory, Salu. Castor ni mwanafunzi wa mwaka wa pili katika shahada ya kwanza ya fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma. Maelezo haya ameyatoa tarehe 21/02/2020 alipofanya mazungumzo na mtafiti.

Mimi nimesimama kama ngongoti

Ujumbe unaotokana na taswira za wimbo wa 'Salome' unawashawishi vijana wadogo ambao ndio washabiki wa nyimbo hizo kwa kiasi kikubwa kufanya yale ambayo yameelezewa katika mistari ya wimbo. Vilevile tunaona katika wimbo wa 'Nasema Nawe' katika mistari ifuatayo:

Kata kiuno chako mwenyewe (kata)
Mola amekupa wewe (kata)
Tena vya kili kilali (kata)
Nipe vya **bara** na **pwani** (kata)
Vile vya nje na ndani (kata)

Lugha ya taswira iliyotumika inahamasisha hadhira kufanya matendo hayo kutokana na hisia zitokanazo na maneno hayo. Vilevile, taswira ya bara na pwani katika muktadha wa ufanyaji wa mapenzi kunaashiria namna mbili za ufanyaji wa mapenzi ambazo ni kinyume na miiko ya kitamaduni na kidini. Utumiaji wa taswira kwa namna hii huwashawishi zaidi vijana kufanya yote yanayoimbwa na kusemwa na wasanii hawa. Matokeo ya majaribio ni kujiingiza katika matendo ya ngono kabla ya wakati maalumu na kuweza kupata mimba au magonjwa ya zinaa katika umri mdogo. Nyimbo nyingine hushawishi hadhira kujiingiza katika matumizi ya vileo, madawa ya kulevya au mapenzi ya kinyume cha maumbile.

#### 4.4.2.3 Husabisha Utata wa Maana

Taswira ni kati ya vipengele vya lugha vinavyobeba maana tata katika mawasiliano[9]. Vipengele vingine vinavyoweza kusababisha utata ni matumizi ya misimu, maneno yenye maana zaidi ya moja, kwa kutaja vichache. Tasinifu hii imebaini kuwa wasikilizaji wengi walikuwa na maana tofautitofauti ya taswira moja walizobaini katika nyimbo tafitiwa. Hivyo, utata unaobebwa na taswira, unaweza kuwa kikwazo cha wasikilizaji wa muziki huu kuelewa ni nini hasa kilichokusudiwa na msanii katika nyimbo husika. Uelewekaji wa taswira zinazojidhihirisha katika nyimbo za Mrisho Mpoto husababisha utata katika kueleweka kwake, mfano katika wimbo wa 'Chocheeni':

Chocheeni kuni mbichi,

[9] Maelezo haya yametolewa na Bw. Wilson, Alkado. Wilson ni mwanafunzi wa mwaka wa pili katika shahada ya kwanza ya fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma. Maelezo haya ameyatoa tarehe 21/02/2020 alipofanya mazungumzo na mtafiti.

Moto ukoleee, ugali uive,
Mnacho taka kitokee
Alikeni mamluki,
Wakija wangojee, mikeka wawekee
Wanachotaka kitokee.

Maana ya taswira zilizotumika katika mistari ya wimbo huu huleta utata katika kupata maana yake kwa hadhira. Taswira kama kuni, moto, mikeka na ugali huleta maana tata kwa hadhira kulingana na uelewa wa hadhira husika. Hata hivyo, utata wa maana wa taswira zitumikazo katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya unaweza kuondolewa kwa wasikilizaji kuzingatia kwa umakini vidokezo vinavyotajwa na taswira husika kwa pamoja na maneno mengine ya wimbo mzima kwa kuhusianisha na mazingira halisi yanayomzunguka msanii na jamii husika ili kupata taswira sahihi inayokusudiwa na msanii husika.

**4.5 Muhtasari wa Sura ya Nne**

Sura hii imejadili matokeo ya utafiti kuhusu Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya. Sura hii imejadili taswira zinazojitokeza katika nyimbo za wasanii tafitiwa, athari za matumizi ya taswira hizo na mwisho ni dhima ya matumizi ya taswira katika tungo za muziki huo. Aidha, tasinifu hii imebainisha kuwa, Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya yana athari chanya na athari hasi. Vilevile, tasinifu hii imeonesha kuwa, zipo dhima kadha wa kadha zinazowasukuma wasanii kutumia taswira katika kazi zao. Pamoja na matokeo haya ya utafiti, tasinifu imebaini kuwa wasikilizaji wengi wa muziki huu ambao ni vijana na watoto, wanashindwa kuzielewa baadhi ya taswira zitumikazo katika tungo husika na kushindwa kuelewa kusudi la msanii katika taswira hizo.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Utafiti wetu uliozaa tasinifu hii ulihusu Dhima za Taswira katika Nyimbo teule za muziki wa kizazi kipya za Diamond Platnumz na Mrisho Mpoto. Kwa kuwa utafiti wetu ulitambua kuwa wasanii husika wana nyimbo nyingi na isingewezekana kuzitafiti zote, tulitumia sampuli ya nyimbo tano kwa kila mmoja na kuongoza na nadharia ya semiotiki. Katika sura hii tumewasilisha muhtasari wa tasinifu, mapendekezo na hitimisho kuhusiana na tasinifu hii. Hivyo, sura hii inaanza kwa kuwasilisha muhtsari wa tasinifu na kufuatiwa na hitimisho pamoja na mapendekezo ambayo nayo yamegawanyika katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza ya mapendekezo ni mapendekezo kwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya. Pili, ni mapendekezo kwa jamii. Tatu, ni mapendekezo kwa serikali. Nne na mwisho, ni mapendekezo kwa tafiti zijazo.

## 5.2 Muhtasari waTasinifu

Tasinifu hii imegawanyika katika sura tano. Sura ya Kwanza inahusu utangulizi ambayo imetambulisha usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo na utafiti, malengo, maswali ya utafiti na umuhimu wa utafiti. Sura ya Pili iinahusu mapitio ya maandiko na nadharia iliyozotumika kama mwega wa utafiti. Sura ya Tatu ni Usanifu na mbinu za utafiti ambayo imefafanua mbinu za utafiti pamoja na uwasilishaji na zana mbalimbali zilizotumika katika utafiti; ukusanyaji pamoja na uchambuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Vipengele vilivyofafanuliwa ni mpango wa utafiti, eneo la utafiti taarifa za walengwa wa utafiti, vifaa vya kukusanyia data pamoja na udhibiti na uthabiti wa data. Sura ya Nne ni mjadala wa matokeo ya utafiti ambayo imejumuisha suala la uchanganuzi wa data na mjadala wa matokeo ya utafiti. Hapa kila lengo mahususi limejadiliwa. Sura ya Tano ni muhtasari, hitimisho na mapendekezo. Aidha kuna viambatisho mbalimbali vinavyohusiana na utafiti huu.

## 5.3 Hitimisho

Tasinifu hii iliongozwa na malengo matatu ambayo ni; kubaini taswira zinazojitokeza katika nyimbo husika, kubaini athari za matumizi ya taswira na kubaini dhima za matumizi ya taswira katika nyimbo teule. Tasinifu hii imebaini kwamba nyimbo za wasanii wa muziki wa kizazi kipya zimesheni taswira

mbalimbali. Kwa upande wa dhima ya taswira, tasinifu hii imebaini kuwa taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya hutumika kwa dhima zifuatazo: kukwepa udhibiti wa kazi zao; kufikisha ujumbe; kuonesha ufundi wa kisanaa; kuivutia hadhira; kuburudisha jamii na kupamba kazi za msanii. Aidha Nadharia ya Semiotiki imesaidia kutambua namna taswira zinavyojitokeza na maana zinazobebwa na taswira hizo kwa kuchunguza ishara, alama na vidokezo vya kitaswira kwa kuangalia uhusiano wake na kitu husika ili kupata maana sahihi ya taswira.

Aidha, tasinifu hii imebaini kuwa kuna athari chanya na hasi za matumizi ya taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya. Athari chanya zilizobainika ni: kuibua hisia za hadhira; kukuza udadisi wa hadhira; kuchochea wimbo kupendwa; hufanya ujumbe kueleweka kwa urahisi; kukuza lugha lugha na kudumisha maadili ya jamii. Athari hasi zilizobainika ni: husababisha uelewekaji mbaya wa nyimbo; huharibu lugha/msamiati; husababisha ugumu wa kupata undani wa ujumbe uliokusudiwa na msanii; hochochea mmomonyoko wa maadili na kusababisha utata wa maana. Kutokana na matokeo ni dhahiri kuwa pamoja na athari za matumizi ya taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya, zipo dhima zinazobebwa na matumizi ya taswira hizo. Ni kazi ya wasikilizaji wa muziki huo kuzichunguza taswira na kuelewa maana zake.

## 5.4 Mapendekezo

Kutokana na tasinifu hii, mtafiti anapendekeza kwa makundi mbalimbali yanayohusika na aina hii ya muziki yafanye yafuatayo:

### 5.4.1 Mapendekezo kwa Wasanii wa Muziki wa Kizazi Kipya

Mtafiti anapendekeza wasanii wajikite kutumia taswira zinazoeleweka vizuri na zinazozingatia maadili ya jamii ili jamii iweze kunufaika zaidi na ujumbe unaobebwa na muziki huu.

### 5.4.2 Mapendekezo kwa Jamii

Jamii inatakiwa kuzama zaidi katika kupambanua maana zinazobebwa na taswira hizo ili kujua kinachozungumziwa hasa na taswira hizo. Hii itasaidia jamii kutokujiimbia hovyo mitaani au mbele ya watu wanaowaheshimu nyimbo zinazobeba taswira zisizozingatia maadili.

### 5.4.3 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Tafiti nyingi zaidi zinatakiwa kufanyika kuhusiana na nyimbo za muziki wa kizazi kipya, hususani katika vipengele vingine vya lugha. Hii ni kutokana na ukweli kwamba muziki wa sasa wa kizazi kipya kudaiwa kuwa na matumizi ya lugha yasiyofaa kwa jamii.

Japokuwa tasinifu hii imeziba mwanya uliolengwa kuzibwa lakini bado kuna sehemu ambazo zinapaswa kufanyiwa uchunguzi na utafiti wa kina, sehemu hizo ni:

i: Matumizi ya taswira katika nyimbo za wasanii wengine wa muziki wa kizazi kipya..

ii: Nafasi ya taswira katika kupamba nyimbo za muziki wa kizazi kipya .

iii: Taswira kama nyenzo ya kuficha udunishaji wa mwanamke katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya. .

# MAREJELEO


Badru, Z. A. (2011). Dhima ya Taswira na Mabadiliko yake katika Vitendawili: Mfano wa Vitendawili vya Kiswahili: Tasinifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma. Dodoma (Haijachapishwa).

Badru, Z. A. (2015). Taswira na Ubainishaji wa Mabadiliko ya Kiujumi Katika Vitendawili: Mfano wa Vitendawili vya Kiswahili: Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma. Dodoma.

BAKIZA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Longhorn Publishers Tanzania

Barthes, R. (1968). *Element of Semiology*. New York: Hill and Wang.

Cohen, L na Wenzake (2007). *Research Methods in Education 16 Edition*. London: Routledge

Chachage, S. (2002). "Ndani ya Bongo: Utandawazi na Migogoro ya Utamaduni." Makala iliyowasilishwa katika Mkutano wa Kumi wa Hali ya Siasa Tanzania. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam.

Chandler, D. (2005). Semiotics for Beginners. Aberyswyth University. Inapatikana: http://www.aber.ac.uk/media/Documents/S4/semo1.html. Imesomwa Agosti 18, 2019.

Creswell, J.W. (2012). *Educational Research: Planning, Conducting and Evalueting Quantitativeand Qualitative Research.* Boston: Pearson Education.

Dey, I. (2005). Qualitative Data Analysis: A user Friendly Guide for Social Scientist. Tylor & Francis e-library.

Eco, U. (1976). *A Theory of Semiotics*. Indiana: Indiana University Press.

Frey, L, Botan,C & Kreps,G (1999). *Investigating Communication: An Introduction to Research Methods*. Boston:Allyn & Bacon.

Fenn, J. & Perullo (2000). "Language Choice and Hip Hop Scene in Tanzania and Malawi" Katika Popular Music and Society, imepakuliwa kutoka, https://www.researchgate.net/publication/233034267, imesomwa tarehe 29/07/ 2019.

Hawkes, T. (1997). *Structuralism and Semiotics*. London: Methuen Co Ltd.

Jilala, H. (2010). "Lugha na Jinsia katika Ushairi: Uchunguzi wa Sitiari za UKIMWI na Mapenzi katika Mashairi ya Bongo Fleva". Mulika. Uk.55-68. Dar es Salaam: TUKI.

Jumbe, A. H. (2015). "Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya: Mfano kutoka katika Nyimbo za Mapenzi za Wasanii Inspekta Haroun na Mwanafalsa." Tasinifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kasege, U. (2013). "Matumizi ya Lugha Yanavyoibua Dhamira za Kisiasa katika Diwani ya Fungate ya Uhuru (1988) na Wasakatonge (2003)." Tasinifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu

Kombo D. K na Tromp D.L.A (2006). *Proposal and Thesis Writing*: An Introduction. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology; Methods and Techniques*. New Age International (P) LTD.

Lanham, R. A. (1991). *A handlist of Rhetorical Terms*. Calfonia: Calfonia Press.

Majembe, A. K. (1998). "Language Use in the Tanzanian Hip Hop Scene", Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mangesho, P. (2003). "Global Cultural Trend. The case of Hip Hop Music inDar es Salaam", Tasinifu ya kwaajili ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma.

Massamba D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Masungwa, S. T (2012). Taswira na Ishara katika Ushairi wa Mathias Mnyampala. Tasinifu kwa ajili ya shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma.

Maxwell, J.A. (1996). Qualitative Research Design: An Interactive approach, Tgousand Oaks, Sage publications.

McKee, Alan (2001). A Beginner's Guide to Textual Analysis. Queensland University of Technology. Metro Magazine. 138-149. Imepakuliwa kutoka http://eprints.qut.edu.au/41993

Mulokozi, M. M na Kahigi, K.K. (1973). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*.Dar es Salaam: TPH

Mwari, A. (2016). "Taswira za Hali na Maana katika Nyimbo za Kizazi Kipya: Kundi la Offside Trick." Katika *Mulika 2017 Toleo Maalumu*. Dar es Salaam: TATAKI.

Mzee, A. F. (2011). Athari za Nyimbo za Taarabu ya Mipasho Katika Jamii ya Wazanzibar. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri Chuo Kikuu cha Dodoma: Dodoma.

Nauta, D. Jr. (1972). *The Meaning of Information*. The Haque: Mouton

Njogu, K. na Chimerah, R . (2008). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Omari, S (2006). "Mitindo na Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya Tanzania".*Kiswahili. Juz.69*. uk. 73-92. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Omari, S. (2009). "Tanzania Hip Hop Poetry Literature", Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Omari, S. (2011). “The Role of Slang in Understanding Bongo flava Content and Culture, in Readings in Ethnomusicology”, University of Dar es Salaam: Dar es Salaam.

Omari, S. (2013). “Hip Hop Music as a Youth Medium for Cultural Struggle in Zanzibar”, The Journal of Pan African Studies, vol.6, No.3. imepakuliwa https://www.questia.com/library/journal/1G1-347293086/hip-hop-music-as-a-youth-medium-for-cultural-struggle imesomwa tarehe 29/07/2019.

Ponera A. S (2014). “Ufutuhi katika Nathari za Kiswahili: Ulinganisho wa Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi”, Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Ponera A. S (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Remes, P. (1999). “Global Popular Musics and Changing Awereness of Urban Tanzania Youth,” katika Year book for Traditional Muzic, Vol. 31 (1999), uk.1-26. International Council for Traditional Music.

Samwel, M. (2012). “Mabadiliko katika Majigambo: Uchunguzi wa Majigambo ya Jadi na ya Bongo Fleva”, Phd. Tasinifu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Selanda, Z (2018). Vionjo vya Fasihi ya Kisasa katika Nyimbo Teule za Singeli: Tasinifu ya shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma.

Selden, R. (1985). *An Introduction to Literary Criticism*. New York: Harvester

Senkoro,F. E. M. K. (1983). *Fasihi*.Dar es Salaam: Press and Publicity

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Ushairi, Nadharia na Tahakiki*.Dar es Salaam: DUP

Simon, K. B. (2014). Ishara katika Kaptula la Marx na Kijiba cha Moyo: Mtazamo wa Kisemiotiki: Tasinifu ya shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Nairobi.

Suriano, M. (2006). “Hip Hop and Bongo Flavour Music in Contemporary Tanzania: Youth’ Experiences, Agency, Aspirations and Contradictions.” Imepakuliwa kutoka www.ascleiden.nl/pdf/youthconfsuriano1.pdf. Imesomwa tarehe 29/07/2019

Tandiko, N. (2015). Dhima ya Taswira katika Nahau za Kisambaa. Tasinifu ya shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma.

TUKI (2011). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press

Venance, F. (2017). “Dhamira za Kisiasa katika Mashairi ya Bongo Hip Hop na Jinsi zinavyoakisi Jamii: Uchambuzi wa Mashairi ya Joseph Mbilinyi (Sugu) na Ibrahimu Musa (Roma).” Tasinifu ya Shahada ya Umahiri katika Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W.  (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Wheatsheaf.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi: Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

## VIAMBATANISHO

A: ORODHA YA WATAFITIWA – WALIOFANYIWA USAILI

A. 1 : Wasikilizaji wa muziki wa kizazi kipya wenye Umri kati ya miaka 17-35

| JINA | JINSI | UMRI | MAHALI | TAREHE YA USAILI |
|---|---|---|---|---|
| Peace Manyilizu | KE | 31 | Chanika-DSM | 16/03/2020 |
| Dafroza Luhaga | KE | 32 | Goba-DSM | 16/03/2020 |
| Schola Samwel | KE | 27 | Mbezi-DSM | 18/03/2020 |
| Festo Dickson | ME | 23 | Mbezi- DSM | 18/03/2020 |
| Michael Elius<br>Daima Swai | ME<br>KE | 29<br>27 | Tegeta-DSM<br>Tegeta- DSM | 19/03/2020<br>19/03/2020 |
| Haule | ME | 32 | Ubungo-DSM | 21/03/2020 |
| Yohana Sasi<br>Julieth Fransis<br>Abdalah Nzoa | ME<br>KE<br>ME | 19<br>31<br>28 | Ubungo-DSM<br>Tabata bima-<br>DSM | 21/03/2020<br>22/03/2020<br>22/03/2020 |
| Yusufu Shitenge | ME | 25 | DODOMA | 02/04/2020 |
| Chege | ME | 31 | DODOMA | 02/04/2020 |
| Tiffa | KE | 19 | DODOMA | 02/04/2020 |
| Salma Abdalah | KE | 23 | DODOMA | 04/04/2020 |
| Hosiana Lyimo | KE | 18 | DODOMA | 04/04/2020 |
| John Magway | ME | 24 | DODOMA | 05/04/2020 |
| Stecy Kimario | KE | 32 | DODOMA | 05/04/2020 |
| Jane Mbangali | KE | 29 | DODOMA | 07/04/2020 |
| Venance Mavunde | ME | 28 | DODOMA | 09/04/2020 |
| Jonathan Steven | ME | 27 | DODOMA | 09/04/2020 |

A.2 Wanafunzi wa mwaka wa pili, wa shahada ya kwanza katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma waliofanyiwa usaili

| JINA | JINSIA | NAMBA YA USAJILI | TAREHE YA USAILI |
|---|---|---|---|
| Shirima, Magreth | KE | T/UDOM/2018/09383 | 21/02/2020 |
| Jackson, John | ME | T/UDOM/2018/09997 | 21/02/2020 |
| Wilson, Alkado | ME | T/UDOM/2018/14479 | 21/02/2020 |
| Castory, Salu | ME | T/UDOM/2018/10759 | 21/02/2020 |

A.3 Madjei waliofanyiwa usaili

| JINA | TAREHE YA USAILI |
|---|---|
| DJ Luba | 07/04/2020 |
| DJ Sk | 07/04/2020 |
| DJ Homeboy | 08/04/2020 |
| DJ Soliso | 10/04/2020 |
| DJ Kacha | 10/04/2020 |

B. Barua ya ruhusa ya kufanyia utafiti

**CHUO KIKUU CHA DODOMA**
**OFISI YA MAKAMU MKUU WA CHUO**

P.O. BOX 259
DODOMA, TANZANIA [illegible]

**Kumb. Na. UDOM/RP/68Vol. IV /16** **Tarehe: 23 Machi, 2020**

Katibu Tawala wa Mkoa
**Mkoa wa Dodoma.**

Katibu Tawala wa Mkoa
**Mkoa wa Dar es Salaam**

**YAH: IDHINI YA KUFANYA UTAFITI**

Dhumuni la barua hii ni kumtambulisha **Bi. Mgalula Sarah** ambaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma mwenye namban ya usajili **HD/UDOM/00059/T.2018**. Mwanafunzi wetu amefikia hatua ya kufanya utafiti kama sehemu ya mafunzo katika kozi (programu) husika.

Kwa mujibu wa waraka wa Serikali wenye Kumb: Na. MPEC/R/10/1 wa tarehe 4 Julai, 1980, Makamu Mkuu wa Chuo amepewa mamlaka ya kutoa idhini ya kufanya utafiti kwa watumishi na wanafunzi wa Chuo Kikuu kwa niaba ya Serikali na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH). Hivyo ninapenda kukuarifu kuwa nimetoa idhini ya utafiti kwa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu.

Aidha ninakuomba umpatie msaada wowote utakaohitaji kufikia malengo ya utafiti wake. Zaidi tunakuomba umruhusu mwanafunzi wetu kuonana na kuzungumza na Wanafunzi wa Mwaka wa pili wa shahada ya kwanza katika fasihi ya Kiswahili wa Chuo kikuu cha Dodoma, Madijei, wasikilizaji na Matini mbalimbali muhimu kwa utafiti wake katika Mkoa wako.

Mada ya utafiti wake ni ***"Dhima ya Taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya: Mifano kutoka kwa Nasibu Abdul (Diamond Platium) na Mrisho Mpoto"***

Kipindi cha utafiti wake ni kuanzia Aprili hadi Julai, 2020 na utafanyika maeneo ya Dodoma na Dar es Salaam- atazungumza Wanafunzi wa Mwaka wa pili wa shahada ya kwanza katika fasihi ya Kiswahili wa Chuo kikuu cha Dodoma, Madijei, wasikilizaji, na Matini mbalimbali kuhusiana na utafiti huo.

Kama kuna pingamizi lolote unaombwa kutushauri ipasavyo. Kwa taarifa zaidi usisite kuwasiliana nasi kupitia kurugenzi ya Utafiti, Machapisho, Ushauri na Ushirikiano wa Kitaasisi S. L. P. 251, Dodoma. Namba ya simu + (255) 262310301, Barua pepe:research@udom.ac.tz.

Wako katika ujenzi wa Taifa,

VICE CHANCELLOR
THE UNIVERSITY OF DODOMA
P. O. BOX 259
DODOMA, TANZANIA

Prof. Faustine K. Bee
**MAKAMU MKUU WA CHUO**

## C. PICHA MBALIMBALI ZINAZOHUSIANA NA UTAFITI



C.1 Picha ya watafitiwa (wanafunzi) walipofanya mahojiano na mtafitiwa katika Chuo Kikuu cha Dodoma.



C.2 Picha ya watafitiwa (wanafunzi) walipofanya mahojiano na mtafitiwa Chuo Kikuu cha Dodoma.

## D. Nyimbo Teule

### D.1 Nyimbo za Nasibu Abdul (Daimond)

#### D.1.1 Iyena (Diamond na Rayvany)

Ah Leo Chereko Chereko
Mwanenu nimekuwa
Zile kuringa mideko itapungua
Ahsante mama ulinifunza nkajua
Baba kasema kuomba mwiko
Raha ya chumvi kununua
Tena si kwa nazi
Si hirizi za waganga
Kwa baraka za baba na mama
Tu na dua
Waambie paparazi
Pingamizi wenye viranga
Waliosema hayawi hayawi yamekuwa

Iyena Iyena
Iyena Iyena
Iyena Iyena
Kwaheri tutaonana
Iyena Iyena

Iyena Iyena
Iyena Iyena
Ntawakumbuka sana

Ooh.. Ndoa baraka
Ukipata ushukuru
Maana wanayoililia ni wengi sana
Kwetu talaka
Kuitoa ni kufuru
Nimefunzwa vumilia
Niushinde ujana
Ili kesho mahususi
Kusudi wasinong'one
Embu nichumu niringe washushuke
Na hii pete ya harusi
Nakuvisha waone
Wakale sumu
Wavimbe wapasuke

[Diamond Platnumz & Rayvanny:]
Ati nashika nanga
Nteke nsichomoke ndani (Anameremeta)
Futa namba wablock vimada wa zamani (Anameremeta)
Sio vijembe vya kanga waziwazi mambo hadharani (Anameremeta)
Waliopanga mwenye nyumba kaja ndani (Anameremeta)

[Diamond Platnumz:]
Iyena Iyena
Iyena Iyena
Iyena Iyena
Kwaheri tutaonana (Oh, kwaheri baba mama)
Iyena Iyena
Iyena Iyena
Iyena Iyena
Ntawakumbuka sana

[Rayvanny:]
Imefika tamati
Tulisubiri kitambo
Leo samaki
Kanasa kwenye chambo
Pongezi kwa kamati
Yanavutia mapambo
Napata picha safi
Litanikoma bundle
Mwanamke usafi
Gaga kulisugua
Mume akirudi sharti
Viatu kumvua

Kitandani marashi
Massage kumchua
Kisha anza sayansi
Viuno kutengua
Mambo ya kuzima taa
Si mahaba ni kuwanga
Washa japo ka mshumaa
Mumeo aone shanga

Makeup kinanda
Kaka suit kama mbunge (Anameremeta)
Mulo changa muda kujipooza na punje (Anameremeta)
Momo ndani Shivo amekuja na Fumbwe (Anameremeta)
Kula chanda ukishiba ruksa kafunge (Anameremeta)

[Diamond Platnumz:]
Iyena Iyena
Iyena Iyena
Iyena Iyena
Kwaheri tutaonana (Eh, kwaheri baba mama)
Iyena Iyena
Iyena Iyena
Iyena Iyena
Ntawakumbuka sana

[Diamond Platnumz & Rayvanny:]
Saa nataka kusasambua (Sasambu)
Me nasasambua (Sasambu)
Aby Dad nasasambua mimi (Sasambu)
Sasambua
Tuone
Mguu moja juu (Sasambu)
Usishushe chini (Sasambu)
Cheza jitazame (Sasambu)
Sasambua
Tuone
Aisha kimobitel (Sasambu)
Nipe za baloteli (Sasambu)
Nyonga kibaiskeli (Sasambu)
Sasambua
Tuone
Akaa kama unashika ukuta (Sasambu)
Ifanye unashusha (Sasambu)
Taratibu zungusha (Sasambu)
Sasambua
Tuone
Sasambu! Sasambu! Sasambu!
Sasambua
Tuone

Kama unawasha bajaji (Sasambu)
Imwagie na maji (Sasambu)
Tuwakomeshe vizazi (Sasambu)
Sasambua
Tuone

**D.1.2 Salome (Diamond na Rayvanny)**

Kioo hakidanganyi mama
Umejipodoa umepodoka
Mwendo na shepu, vyote mwanana
Mimi suruali yanidondoka
Tukimbizane nini salome wangu?
Iyo michezo ya jogoo
Mbona watizama chini salome wangu
Ukimuona jongoo
Inama kidogo, shika magoti
Mimi nimesimama kama ngongoti
Mtoto jojo, sio roboti
Chumbani bingili bingili somersault

[Diamond Platnumz:]
Unanitekenyaga ukinyonga Salome
Unanitekenyaga ukinyonga
Unatikenyaga ukinyonga kweli
Unanitekenyaga ukinyonga, aaha
Hoera makulu vane, hoera ngambe
Hoera na Zari, hoera ngambe

Utamu kolea aprokoto
Ting'ali ting'ali ndani kwa moto
Nitamnyongea, msokoto
Niteme sumu kali kama kobokoo
Eeeh Mapenzi yananipa shida
Shida maama, ni donda lisilokuwa na tiba
Tiba bwana, usije baby kanicharanga
Kanichambua moyo kama karanga
Mie baby kwenye msambwanda, huwa sienda
Ngenge ni nganganga

Unanitekenyaga ukinyonga salome
Unanitekenyaga ukinyonga
Unatikenyaga ukinyonga kweli
Unanitekenyaga ukinyonga, aaha
Hoera makulu vane, hoera ngambe
Hoera na Zari, hoera ngambe

[Rayvanny:]
Mie mwenzako nyang'anyang'a
Mie binzari we ndo nyanya

Baby kwangwaru
Isimamie kama kangaroo
Ibane kangwaru
Babu Juma mpige kwa kwaru
Kwakwaru kwakwa

[Diamond Platnumz:]
Chambua kama karanga sasa
Chambua kama karanga
Ichambue kama karanga Salome
Chambua kama karanga
I say washa washa moto washa
Songa songa ugali songa songa
Mpaka chini mpaka chini

[Diamond Platnumz & Rayvanny:]
Wenye wivu wajinyonge leo
Wanye wivu wajiinyonge
Wenye wivu wajinyonge Salome
Wenye wivu wajinyonge
Wenye wivu wajinyonge kweli
Wanakodoa kodo wanakodoa (macho kodo) (wale kodo)
Ukinyonga (wanakodoa kodo wanakodoa)
Ukisonga (wanakodoa kodo wanakodoa)

**D.1.3 Sikomi**

Wanasemaga mapenzi safari
Unavyopita ndo jinsi unajongea
Ila niendako ni mbali sijui ka ntafika sababu natembea
Niliposikiaga habari
Yakisifika nikakesha nangojea
Akabariki jalali na nikawika muziki nikauotea
Ile pruuu mpaka macca
Nikadandiaga bongo movie
Kumbe mapenzi hayataki haraka
Ni kama tango natia tu chumyi
Mwenzenu nikaoza haswa
Na kujitia kitandani mjuzi
Eti nataka fukuza paka
Badala ya mbwa nikafuga mbuzi, hhhmmm

Wivu ukanifanya nikagombana na marafiki
Ugomvi na mamangu akiniambia siambiliki

Moyo ukanambia nasibu sasa mapenzi basi
Ila nang'ang'ania najaribu kuipinga nafsi
Esma ananiambia mdogo wangu mapenzi basi
Ila nang'ang'ania
Nikiumizwa na huyu kesho nina mwingine

Ooh mbona sikomi
Sikomi
Sikomi
Licha ya mateso haya
Najiuliza (oh sikomi)
Oh sikomi mbona (sikomi)
Mbona jamani
Sikomi
Licha ya mateso haya, hhhmmm

Aliyonifanyia wa central
Haki ya mungu siyawezi sema
Ila nimejifunza kesho nisiwaamini wacheza sinema
Moyo walinipatia mateso
Siwezi kumeza siwezi tema
Ndio maana sikushanga ile ghafla
Toka ccm kwenda chadema
Wanasema kitanda ukitandika sharti ukilalie
Nikajitia ukamanda yatakwisha
Wacha nivumilie
Kila kiza kikitanda
Ndo visa machozi me nilie
Penzi yakatia parapanda
Kuwaita waje washambulie

Acha na penny we darling
Nilio muhongaga gari
Aliponambia ana mimba
Mwisho wa siku akaichomoa chali
Mola akanitunuku zari
Akanzalia dume na mwali
Nilivyo mjinga nikacheat aibu mpaka
Kwa vyombo vya habari

Moyo unanambia nasibu sasa mapenzi basi
Ila nang'ang'ania najaribu kuipinga nafsi
Lizer ananiambia simba mapenzi basi
Ila nang'ang'ania
Nikiumizwa na huyu kesho nna mwingine

Ooh mbona sikomi (mbona)
Sikomi (mbona jamani)
Sikomi
Licha ya mateso haya
Eh nishafumania (oh sikomi)
Nikafumaniwa mimi (sikomi)
Nishagombana na watu (sikomi)
Licha ya mateso haya (mateso haya)

### D.1.4 Kanyaga

(Woo, woiyo ooh woiyo ooh)
It's Platnumz, Zombie
(Woo, woiyo ooh woiyo ooh)
It's S2kizzy baby

Ati kanyaga ka ana pigo za unafiki
Kanyaga kama mmbeya asiye rafiki
Kanyaga kama fisi ana roho ya usnichi
Hakulishi, hakuvishi kwani vipi?

Kanyaga
Wazee wa shobo kudandia, kanyaga
Klabu kuomba omba bia, kanyaga
Slay queens vitisho vya bandia
Ukivipa hai ati madai vinavimbia

Kanyaga!
Uzushi, Kanyaga!
Mashemu feki, Kanyaga!
Nuksi, Kanyaga!
Kudadadeki, Kanyaga!
Mawifi, Kanyaga!
Mpaka ma ex, Kanyaga!
Mikosi, Kanyaga!
Woooya Kanyaga!

Kanyaga! Kanyaga!
Kanyaga! Kanyaga!
Kanyaga! Kanyaga!
Kanyaga! Kanyaga!

Yii, Kanyaga! Kanyaga!
Kama unalicheza zanku
Kanyaga! Kanyaga!
Wale wakuda wadaku
Kanyaga! Kanyaga!
Yeah, kidaku daku
Kanyaga! Kanyaga!
Wajue hizi namba chafu

Woo, woiyo ooh woiyo ooh
Woo, woiyo ooh woiyo ooh

Ooh yeah eeh
Siku hizi watu wanataka money
So nikimuita aku kosti, Kanyaga!
Kunitumia mipicha pigo gani?
Ati basi day nikuposti (oh yeah yeah)

Kadi za harusi kuchanga changa, Kanyaga!
Wakati mwenyewe nina majanga, Kanyaga!
Sina godoro sina kitanda
Ati nikuchangie kodi kwenda kupanga (yii)

Kama buti la mugambo, Kanyaga!
Wavuruga mipango, Kanyaga!
Wazee wa Insta michambo
Ati 'baby niunge bando'

Kanyaga!
Uzushi, Kanyaga!
Mashemu feki, Kanyaga!
Nuksi, Kanyaga!
Kudadadeki, Kanyaga!
Mawifi, Kanyaga!
Mpaka ma ex, Kanyaga!
Mikosi, Kanyaga!
Woooya Kanyaga!

Kanyaga! Kanyaga!
Kanyaga! Kanyaga!
Kanyaga! Kanyaga!
Kanyaga! Kanyaga!

Yii, Kanyaga! Kanyaga!
Kama unalicheza zanku
Kanyaga! Kanyaga!
Wale wakuda wadaku
Kanyaga! Kanyaga!

Yeah, kidaku daku
Kanyaga! Kanyaga!
Wajue hizi namba chafu

I say leeeooo...
Usiku hatulali, tunakesha kama popo
Leo, leo
Tena wape na bare, kama wao pakasi kwako

Asa timba, timba timba (timbaaa)
Wanangu timba (timbaaa)
Wao kula kushoto (timbaaa)
Kula kulia (timbaaa)

I say timba, timba timba (timbaaa)
Oyaa wahuni timba (timbaaa)
Kama unazikili (timbaaa)
Mchaka kabisa akili (timbaaa)

**D.1.5 Nasema Nawe**

Halooo…weweee…aaahh kutwa viguru njiani, majirani wote wamekuchoka
Mara chumba cha fulani mtu gani we kwako usiokaa
Washinda vibarazani vya wenzako kuropoka
Ukome mwana fulani ona uso ulivyokukoboka
Sio mwisho vibaoni hadi kwenye vigodoro
Usio na haya usoni kote wazua migogoro
Hivi wee haujioni kuwa una kasoro
Usio mchana jioni si wa juzi si tumoro
Sio mwisho vibaoni kwenye vigodoro
Usio na haya usoni kote wazua migogoro
Hivi we haujioni kuwa una kasoro
Usio mchana jioni si wajuzi si aaah

Kiitikio
Nasema nawe *5
Usio haya nasema nawe,umezoea (nasema nawe)
Chezea chezea (nasema nawe)
Umezidi (nasema nawe)
Zidi (nimechoka nasema nawe)
Huna haya ka kibakuli cha vumba,
Popote unajitokeza,
Babu eee haa we kichoji tu
Unaingia kwenye kundi la niga utachanika mabawa.

Beti ya 2
Mhhh aah zingifuli zingifuli ungezinga mahala ukakaa
Usio mila desturi usiojua tongozwa ukakataa
Usio hiyana fedhuri, uongo umekujaaa
Kujifanya mashuhuri kumbe chaka umechakaaga
Mwenzako mi turufu si garasa mwenye nyota ya umaarufu sikupapasa
Tena jokari la nguvu pakarata lile hodari maguvu si kwasakwasa
Ooohh mwenzako mi ni turufu si garasa mwenye nyota ya umaarufu si hozakoza

Kiitikio
Nasema nawe *5
Usio haya nasema nawe, umezoea (nasema nawe)
Chezea chezea (nasema nawe)
Umezidi (nasema nawe)
Zidi (nimechoka nasema nawe)
Huna haya ka kibakuli cha vumba,
Popote unajitokeza, babu eee haa
Wewee umejifunza ngumi leo wataka upigane na Tyson? Haah

Beti ya 3
Ale kata…kata kakata katika si kata oh teteme….teteme…kataa
Wenye kusema waseme.. kata ale kata kata kakata katika si
Kata kiuno chako mwenyewe (kata)
Mola amekupa wewe (kata)

Tena vya kili kilali (kata)
Nipe vya bara na pwani (kata)
Vile vya nje na ndani (kata)
Tumkomeshe fulani (kata)
Halooo haa utavunjia maepo mwaka huu maana nazi zimepanda bei hahaa heee

Kiitikio
Toa basi ninasema nawe. ona wewe. (nasema nawe)
Nasema nawe usio haya nasema nawe (wewe)
Nasema nawe, nasema nawe, nasema nawe nimechoka nasema nawe
Umezoea nasema nawe, chezea chezea nasema nawe
Ohh nasema naweeee usio haya nasema na wewe
Nasema na wewe, nasema na wewe, nimechoka nasema nawe
Wewe weeaaaah kata…. kata…. kata.

**D.2 Nyimbo za Mrisho Mpoto (Mjomba)**

**D.2.1 Waite**

Waite
Waite wakalishe chini
Watoe hofu kwanza
Wambie wao hawamo
Japo na wao walikula
Waite* 2

Mjomba chutama
Sisi ni waungwana na muungwana
Akivuliwa nguo huchutama
Kuna baadhi ya michezo ukishindana
Peke yako lazima uwe mshindi
Lakini kwa mchezo ule uliwahitaji
Ilikukuongezea mashabiki
Nawashangiliaji wenye sauti zisizo kauka
Japo mwiba wakujichoma hauna pole
Usitenganishwe na mto wakati kuna ngalawa mjomba
Walivyo anza mjomba hakuna aliye dhani
Kwanza walifika mapema
Mmoja wao akaandikisha jina lake
Kwa niaba ya wengine japo wote wana majina yao na hayafanani
Jina lako nani mimi unatoka wapi
Kwetu unakwenda wapi humu ndani
Kikazi au binafsi nani mimi aaaa
Wakaingia haujachelewa mjomba
Waite.

Mjomba ukipewa kuosha maiti,
wewe ni zaidi ya ndugu
wanaamini kwamba huwezi kuizuru
Waliingia wakajipanga kwa sauti zao

Ya kwanza mpaka ya nne
Wakaanzisha mapambio
Basi ikawa hivyo tu
Watu wakilia wanatoa pole
Watu wakilia wana toa pole
Na mwandishi kwa utashi wao wakaandika
Msiba umefana kweli hakuna alie lia nje ya key hehehehehehehehe

Waite
Mjomba ushauri wangu waite
Wakalishe chini
Watoe hofu kwanza
Kisha waambie
Muungwana hanuni kwa mashavu hununa moyoni
Wao hawahusuki wala hawamo
Waje tu kuwa mashahidi
Kwakuwa nao walikuwepo na walikula
Japo kuwa hawakujua umemtoa wapi mbuzi huyo
Ushahidi wao mjomba utakusaidia kwa vitu viwili
Ya kwenye historia au kwenye ushindi
Siku zote mjomba huwa nakuambia
Anaekula kwa mikono miwili hawezi kushiba kamwe
Never
Mimi pia nakumbuka kweli nilimuona
Akikuwa mbuzi tena mdogo tu
Wala sio ngombe kama wanavyo dai
Hii nizawadi tunakupa nenda ukale utukumbuke
Utukumbuke
Leo hii wanasema alikuwa ng'ombe mdogo
Wengine eti oo kweli alikuwa mbuzi
Ila angekuwa ng'ombe
Mjomba kuna aina tatu tu za kujibu
Maswali
Swali kwa swali
Swali kwa maelezo
Swali kwa mkato
Wajibu tu kwa mkato
Alikuwa mbuzi mdogo tumemla akaisha bhaaaasi.

**D.2.2 <u>Chocheeni Kuni</u>**

Hey, yea ooh,
Chocheeni kuni mbichi,
Moto ukoleee, ugali uive,
Mnacho taka kitokee
Alikeni mamluki,
Wakija wangojee, Mikeka wawekee
Wanachotaka kitokee.
Chochea *7
Ooh Chochea,
Chochea *7

Wa Tanzania, mwenda kwao sikuzote haogopi giza,
Acheni nirudi nyumbani, safari imenishinda,
Nauli zenu ntarudisha,
Mtu anatapika nyongo yake,
anailamba tena anaangaliwa,
Ni Sawa na tawi kavu linapoanguka,
Watu wakapiga kelele, ayaa.
Katika misimu minne ya Mwaka,
tuongeze misimu mwingine WA tano, wakujishtusha.
Raha ya jamvi siku zote ni viraka viraka.
Na dungu linamficha mlinzi WA ndege wakati WA mvua tu.
Eti, ooh, imenyesha juzi tu,
Maji sio mengi, nisubirini kule.
Ilishindikana vipi kuyapima maji kwa mti,
Ndo mkawaambia Watu wavuke.
Mjomba, binadamu ni Kama ganda LA kitabu,
paka ufungue maandishi Ndo uweze kumuelewa.
Eti, lililotokea mbali tufanye limepita,
na haliwezi kumdhuru mwingine.
Kweli?!
Inayotaka kunyesha, hua haisubiri mawingu,
Mimi sidhani, Kama kujiponya kwa mambo mzito tunahitaji cheti
kilichigongwa mhuri wa moto au mtaalamu wa magonjwa ya akili,
zaidi yakutumia Neno sahau.
Unawaulizaje Watu magongo ya nini?
wakati Umesema kuna nyoka!
Mjomba, wewe si Uliwapaka wanja,
Ngoja wao wakupake pilipili,
halafu kwenye kimbolela iwe zamu yako kuzinga.

**D.2.3 <u>Njoo Uichukue</u>**

Eeeh eeh
Roho yangu kama itakusaidia (ndugu yangu)
kama itakupa ushindi
Moyo wako najua
Kama itakusaidia kama itakupa ushindi moyo wako najua
Usiku rafiki wa giza
Basi njoo uichukue×3
Uichukue
Basi njoo uichukue×3
Ama kweli kama hujui unapo kwenda huwez kupotea
na watu kukimbia wanakozika hudondokea kwenye maiti nyama.

Siku zote naamin mtu huwez kulala
kwenye mto hata kama umekauka
Na ukitaka kujua mwendo wa mjinga
mpe kilemba uone
Hili niombi langu toka kwangu kuja kwako

Kama ya kwangu itakusaidia chochote kwenye ushindi wako

niko tayari kukupa ila uifuate nyumban wala sio mbali!

Nakukumbusha ukitaka n'zi wasikufuate
Acha kula vilivyooza
chuki humchoma aliyeihifadhi kwenye moyo tu siku zote
Nakuuliza unataka kuja mchana ama jioni
maana kila njia na muda wake najua
mara nyingi ungependa kuja mchana ili uonekane
Naomba nikuelekeze hivi pita uwanja wa taka hadi mfereji mchafu
Kisha kibanda cha mbavu za mbwa katiza usisikie na mtu njiani endelea kuja
Ni kioo tu pekee yake ndo huonyesha doa la kweli kwenye paji la uso
Katiza choo cha gunia pembeni maskani camp Taliban camp
Ukisikia harufu kali bana pua haraka hapo choo kinapakuliwa
na kutia moyo tu njoo karibia unakaribia kufika

Kama itakusaidia (itakusaidia) kama itakupa ushindi (moyo wako najua) ×2
Usiku rafiki wa giza
Uliza baba ubaya aliyetoroka jela au
Mama Mwantum anayesutwa kila kukicha
Ukiogopa kupotea uliza babu Nshuba kikongwe muuza bangi
Atakupa uchochoro utapita ubavu ubavu
Kila hatua utakayopiga kumbuka maji ya dafu hayanywei kwenye glass
Na siku hizi kinachopandwa kwenye changarawe kinakua haraka
Kuliko kwenye udongo
Nakuomba ukisikia kuntumtututu ujue kuna mtu anachezwa
Endelea kuja na ukisikia cherekooo watu wanasasambua
Endelea unakaribia
Alama kubwa utakazokutana nazo ni visheti na chips dume,
Kashata na maandazi, chapati na uroge wa ubuyu,
Pweza na vijiti vyake
Ukiona sufuria la supu unakaribia
Maana nchi yenu nchi yetu pia
Hapa watu pale kinyesi na kondom ndo kwetu
Dampo dogo pale pembeni maji ya mtungi nyumbani huko
Chumba cha baba hapa choo cha pipa pembeni
Unakaribia
Usiponikuta jua ya kwamba nipo ferry
Kuungaunga mwana kwenye samaki
Anayechafua anasafisha kwa kutupa hana hapo sasa umefika
Vipi bado unaitaka na ya kwangu ikuongezee ushindi
Kama ndio kuna masharti mawili tu
Pitia kwa yule mama kamuombe samahani na uumpe pole
Kwa sababu kwa kauli zako alipoteza kitanda chake
Na kwenye hela mkiweka picha zenu wekeni na za kwetu
Wakati mnatumia mtutumia na sisi
Mwisho lakini sio kwa umuhimu
Kwenye kiapo chako cha kweli ongeza na majina yetu
Basi njoo uichukue
Basi njoo uichukue

Basi njoo uichukue (roho yangu)
Basi njoo uichukue
Basi njoo uichukue
Basi njoooo uichukue (Roho yangu)
Basi njoo uichukue uichukue
Basi njooooooooooooooo

**D.2.4 Kitendawili**

Maji ya moto
Kitendawili tega nikutege
Kitendawili tega, tega
Tega nikutege mwiba
Kuku anayetaga hachinjwi, akichinjwa msiba
Sizonjeee
Sizonjee aheee sizonjee
Sizonjeee
Kitendawili
Sizonje aaheee sizonjee
Kumbukumbu yako ikoje katika kukumbuka
Nilikuita sizonje ili uingie ndani
Kwasababu kila anaeingia lazima atoke nje
Sizonje, Sizo Za Nje
Sizonje ahee Sizonjee
Hapa ndipo walipovishana majoho yasiyoonekana
Walisoma hapa, walimaliza hapa
Kila kitu kiliishia hapa
Walipokuja kwetu walituambia
Wale waliosoma na kumaliza
Walimaliza kila kitu wakafa
Kama haujui bahari ilipo tumia mto kwenda

Kitendawili tega, tega
Tega nikutege mwiba
Kuku anayetaga hachinjwi, akichinjwa msiba
Sizonjeee
Sizonjee aheee sizonjee
Sizonjeee
Kitendawili
Sizonje ahee Sizonjeee

Sizonje

Kiukweli watu wanalia
Wapo wanaolia kwa machozi
Na wapo wanaolia kimya kimya
Wapo wanaolia na wanaoendelea kulia
Japo vilio vinatofautiana
Wapo wanaolia kwa kuhisi wamedanganywa
Wapo wanaolia kupoteza ndugu zao
Lakina wapo wanaolia kuona kuna msiba kwao

Lakini marehemu ndio muandaaji
Wali mweupe kwa shekheee, msiweke nyama za mifupaaaa
Watoto kaeni wanne wanneeee, waandaaji tutakula uwani tena mwishoo!
Shida zilipohamia shuleni, nikaona nikuwahi kidogo Sizonje.
Mtoto anapoulizwa "Nani atalipa ada?", "baba!""Yuko wapi??", "kafa!"
Mwalimu wa fasihi anapotoa mfano wa maiti maiti zinazotembea,
Wale watoto wanalia tena
Kwahiyo Sizoo,
Huku nje watu wote wanalia tofauti Lakini msiba ni mmoja
Unaonaje, tuzike kwanza au tuhesabu idadi ya maiti zinazotembea?

Kitendawili tega
Tega nikutege mwiba
Kuku anayetaga hachinjwi, akichinjwa msiba
Sizonjeee
Sizonjee aheee sizonjee
Sizonjeee
Kitendawili

Sizonje aheee Sizonjeee
Sizonje

Naomba ikumbukwe kwamba, aliyemfundisha Chui kula watu ni binadamu.
Na anayekunyoshea kidole
Kuwanaye makini naye sio muda mrefu atakunasa kofi.
(Sizonje)
Kuku ana hatua tatu katika ukuaji wake
Huachwa kwanza atage, ujue utagaji na wingi wa mayai yake
Tunamsubili atotoe tuhesabu vifaranga na mayai viza
Ndugu zangu, inawezekana kweli tumechoka maharage
Lakini kama tunataka nyama tusubirini kwanza banda lijae.

Kitendawili tega, tega
Tega nikutege mwiba
Kuku anayetaga hachinjwi, akichinjwa msiba
Sizonjeee
Sizonjee aheee sizonjee
Sizonjeee
Kitendawili
Sizonje aheee sizonjee
Sizonje

D.2.5 Sizonje

Sizonje hii ndio nyumba yetu
Milango ipo wanapita madirishani
Sizonje ndio nyumba yetu milango ipo wanapita madirishani
Ingia uyaone maajabu ya nyumba yetu, ingia uyaone maajabu ya nyumba yetu
Tulikaa barazani, tukasikia kelele toka ndani
Mtu anaruka dirishani, sizonje karibu nyumbani kwetu

Uone maajabu ya nyumba yetu
Karibu sana Sizonje, hi indo nyumba yetu
Tulipoficha mundu za kupondea wezi, kwani,
Makaburi yaliofukuliwa lazima yazikwe upya?
Nyumba hii sizonje ina vyumba vinne
Vitatu havifunguki, kimoja hakina mlango, japokuwa kina watu ndani
Hawaongei Kiswahili, wenyeji wanalala sebleni na walishazoea.
Sizonje kule tulipotoka panaitwa jikoni
Huna haja ya kwenda kule, kumejaa mafundi wa kupika
Sasa hivi wanakupikia wewe ili ule ulale
Ukiamka muongee nini hasa ujio na dhima ya safari yako
Wanashangaa mbona gafla, samahani sana mgeni
Wapishi wameniomba kwamba nikuulize tena kwa kukuomba kwamba
Eti unapendavya mafuta au vya nazi
Wanataka kukuonyesha madoido katika mapishi yao
Sizonje chumba hiki naomba usiingie ukimaliza ntakwambia kwanini
Kuna sauti inajirudia mara kwa mara
Na hapa mlangoni kulikuwa na picha mbili kubwa
Moja picha, nyingine mchoro wa picha wa kwanza
Ninachokumbuka iliwahi kuandikwa usiyemtaka kaja
Hatukuwahi kuelewa maana yake,
Labda kwasababu ya ujio wako unaweza kutusaidia

**Kiitikio**
Sizonje hii ndio nyumba yetu
Milango ipo wanapita madirishani
Sizonje hii ndio nyumba yetu
Milango ipo wanapita madirishani
Ingia uyaone, maajabu ya nyumba yetu.

Beti ya 2
Najua, wimbo mbaya haufai kubembelezea mtoto
Na kamwe mtoto hawezi kuungua
Kwa kiazi kilichokuwa kwenye kiganja cha mama yake mzazi
Njoo huku uone, sizonje si unajua, harufu ya uzazi haiishi,
Mpaka mtoto akue. Sawa sizonje, huu hapa ni ua
Lile pale ni shimo la taka, na kile pale ni choo
Kinachotutisha na kutuogopesha zaidi
Wanaoishi humu ndani hawajawahi kutupa taka wala kwenda chooni
Kama ukiwa makini kwa nje utasikia sauti za makundi ya watu
Wengi ni vijana, wana bahasha za khaki mikononi
Kama hamtupi taka shimo hili mlichimba la nini lakini pia kwenye sauti zao,
Sizonje kuna watoto, wazee na kina mama ukiunganisha sauti zao
Ndio unapata hizo kelele, ninavyosikia
Ila sina uhakika waliambiwa kihistoria nyumba hii ni ya kwao.
Na wana haki ya kutupa taka na kutumia choo hiki. Sasa
Njoo nikuonyeshe huku uchochoroni uone maajabu mengine
Ya nyumba hii sizonje, ukiona tembo anaringa
Ujue mvua zinakaribia

Kiitikio

Sizonje hii ndio nyumba yetu
Milango ipo wanapita madirishani
Sizonje hii ndio nyumba yetu
Milango ipo wanapita madirishani
Ingia uyaone, maajabu ya nyumba yetu,
Ingia uyaone, maajabu ya nyumba yetu,
Ingia uyaone maajabu ya nyumba yetu.

**E: Mwongozo wa usaili**

E.1 Mwongozo wa usaili kwa madijei na wasikilizaji wa muziki wa kizazi kipya

Je, umewahi kusikiliza nyimbo za Mrisho Mpoto na Nasibu Abdul

- Taswira zina umuhimu gani katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya?

E.2 Mwongozo wa usaili kwa wanafunzi wa mwaka wa pili wa shahada ya kwanza katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma.

- Unadhani matumizi ya taswira yana umuhimu wowote katika kazi za kifasihi
- Unafikiri ni athari zipi zitokanazo na matumizi ya taswira katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya.